# *Kiu*

Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa makuu kuwa hapa usiku wa leo. Hii ndiyo mara yangu ya pili kuwa katika hili Kusanyiko la Grantway, pamoja na Ndugu yangu mpendwa Mack na hawa wafanyi kazi wema hapa, na Wakristo waliounganika nao kutoka makanisa mbalimbali. Ndugu Lee Vayle. Nami ndiyo kwanza nikutane na ndugu fulani hapa, ambaye ni rafiki m—msiri wa F.F. Bosworth, naye hata hakujua Ndugu Bosworth alikuwa amesha kwenda kuwa pamoja na Bwana. Nikasema, "Najisikia kama nimekutana na Elisha aliyemwagia mikono ya Eliya maji," walipokuwa ng'ambo na hawakujua ya kwamba Ndugu Bosworth aliisha kwenda kuwa pamoja na Bwana, akiwa na umri wa miaka themanini na minane.

2 Sasa nataka kuwasalimu watu walioko kwenye simu usiku wa leo, kote nchini, kote kutoka California hadi New York, na Texas na—na kote mahali mbali mbali taifani, kutoka Maine hadi California. Kwa hivyo tuna nji—njia ya mawasiliano ya hizi simu, ambayo imekuwa yenye baraka kuu. Na sasa tunafahamu, kupitia kwa rafiki yetu mwema, Ndugu Pearry Green, ya kwamba wana—wana chombo kidogo wanachoweza kuingiza kwenye televisheni yako, na haitakuwa tu kwa simu, bali yote yataonyeshwa katika chombo chako cha televisheni, pia. Nao wanakitayarisha sasa.

3 Na, Dada Mack, nina furaha kukuona ukionekana mzima, ukiketi hapa kwenye kinada, usiku wa leo. Na wengi wa marafiki wangu nawaona kutoka kule Sierra Vista, na Ndugu Borders . . . ama Ndugu Roberson, namaanisha, kutoka Indiana; wengi. Nataka kuwaambia watu wa kule Maskanini, usiku wa leo, yaonekana kana kwamba nusu yao wako humu, na kutoka kwenye Maskani kule Jeffersonville.

4 Na kwa rafiki yangu kule, Ndugu Koontz, uliyenipigia simu, kuhusu yule mgonjwa, haja hiyo. Ninaomba kwa ajili yake, Ndugu Koontz. Amini tu. Usifadhaike. Itakuwa sawa.

5 Na kule Texas, Ndugu Blair, iwapo unasikiza usiku wa leo, ndugu yangu, kumbuka tu hili; ya kwamba Mungu aliyekuponya mara ya kwanza, aweza kukuponya mara ya pili. Nasi tunaamini ya kwamba Mungu atakujalia hili. Nawe usiuamini uongo wa Shetani kuhusu cho chote. Kumbuka tu ya kwamba Mungu ni Mungu, na kuna . . . naye yungali anadumu yeye yule jana, leo, na hata milele. Nasi tunampenda na kumwamini, na tunakuombea.

6 Marafiki wetu wote kule California, na kwa Ndugu Mercier na wengineo huku Arizona, mahali pengine pengi, Phoenix; na Ndugu Williams, nanyi nyote mnaosikiza kwa simu kule

usiku wa leo, kila mahali, bila shaka tuna furaha; na kule Georgia. Nasi bila shaka tunamshukuru kila mmoja wenu. Bwana awabariki.

7 Ninajisikia nimekaribishwa kabisa hapa usiku wa leo, katika kanisa hili nzuri, Assembly of God hapa Grantway, na pamoja na Ndugu Mack, rafiki msiri wangu. Mungu amembariki Ndugu Mack. Nakumbuka wakati mmoja kule Canada, ya kwamba alikuwa. . .Nilikuwa nimepanda farasi nikifuata mkondo fulani, juu ya farasi; mbali sana kule msituni, kisha Roho Mtakatifu akanena nami kushuka na kumwombea Ndugu Mack. Wakati huo alikuwa hatarini na Bwana alimponya. Na kwa hivyo nashukuru sana kwa hayo, na kukusanyika hapa usiku wa leo pamoja naye, kumwabudu Bwana katika Ukweli huu halisi.

8 Mtu fulani anayeketi jukwaani, nyuma yangu, alisema, "Sidhani unanijua mimi. Kasema, "Wakati mmoja ulinibeba, nilipoomba lifti," kasema, sijui, mahali fulani kule Boston ama po pote pale, "Detroit, nikiomba lifti."

9 Nikasema, "Vema, mimi kwa kawaida hujaribu kuunyosha mkono wangu, nikiweza, kwa wale walio wahitaji."

10 Na kwa hivyo, usiku wa leo, sisi wote ni wahitaji. Nasi tunaomba ya kwamba Mungu atatunyoshea mkono usiku wa leo, wa msaada, na wa baraka, na wa neema Yake pamoja na rehema.

11 Naam, nimezoea kunena kwa muda mrefu, bali nitajaribu kutofanya hivyo usiku wa leo. Maana, watu kule Ohio ndio kwanza wawapigie simu, Bi. Dauch na lile kundi kule, Ndugu Mckinney na Ndugu Brown, na wote wanaosikiza kupitia Ohio. Tunawatumieni salamu, pia. Ni usiku huko New York, nakisia ni saa tano ama saa sita, wakati huu, kule New York. Na makanisa yakaja na kungoja hata wakati huu, kwa ajili ya ibada. Tuna shukrani kwa ajili ya marafiki hao wema kila mahali.

12 Sasa kabla hatujalifungua Neno, hebu na tuzungumze na Mwandishi wake, kwa muda mchache, tunapoinamisha vichwa vyetu.

13 Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, tuna. . .mioyo yetu imejaa furaha, kwa majaliwa tuliyo nayo ya kuwa hai hapa usiku wa leo, na kukusanyika pamoja na watu Wako. Watu. . . na ambao tunaamini wataishi milele. Sasa tuna Uzima wa Milele, kwa maana, "Ulimtoa Mwanao wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele." Katika safari Yake hapa duniani, Yeye alitufundisha, "Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; naye hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa maana tunaamini katika Mwana pekee wa Mungu." Jinsi tunavyokushukuru kwa huyu Mwokozi mkuu! Nasi tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba Uwepo Wake mkuu utatubariki sana hapa, tunaposoma Neno Lake na kunena juu

Yake. Na Roho Mtakatifu aingize hayo kwa kila moyo kote taifani, Bwana, po pote walipokusanyika watu.

14 Wabariki wahudumu wengine walio mimbarani. Tunaomba, Baba, ya kwamba utabariki hili Kusanyiko la Grantway: mchungaji wake, mke wake, watoto wake; mashemasi, wadhamini, na halmashauri yote. Kisha, Baba, sote pamoja na tushughulikie Ufalme wa Mungu, kungaliko na Nuru ya kutosha kuona tunakoenda, kwa maana saa yaja ambapo hapana mtu awezaye kufanya kazi. Pia, Baba, wakati tungali tuna majaliwa haya, na—na tuokoe wakati, Bwana. Na, hebu tujaliwe hayo. Waponye wagonjwa na wanaoteseka kote nchini. Na Uwepo wa Mungu usikike katika kila ufa na pembeni mwa taifa hili, usiku wa leo.

15 Tunatambua ya kwamba hukumu inapiga. Tunajua nyufa kubwa zafanyika chini ya nchi, mataifa yanatetemeka, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Mambo makuu ya kihistoria ambayo tumeyasikia katika siku zilizopita, ya hukumu, kupitia kwa Biblia, nasi tunaona yakitukia tena siku hizi. Unabii ukisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu. Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu," na tunaiona ikitukia sasa. "Watu wakivunjika moyo; fadhaa za wakati, dhiki ya mataifa." Mungu, tunajua ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

16 Tusaidie, Bwana, ku—kusambasa Ujumbe kwenye kila ufa na pembe, kwa kila mtoto ambaye ulimkusudia Uzima. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Bwana, abariki kusomwa sasa kwa Neno Lake.

17 Naam, wengi wenu hupenda kuangalia katika Biblia, ambapo muhudumu anasoma. Nami nataka kusoma usiku wa leo, baadhi yake, vifungu vitatu katika Zaburi. Zaburi 42, kwa ajili tu ya kupata fungu la maneno. Nami nina baadhi ya Maandiko yaliyoandikwa hapa, nami nataka kuyarejea, nikiweza, tunapoendelea katika dakika chache zifuatazo, kunena juu ya somo hili. Zaburi ya Daudi. Daudi aliandika Zaburi.

18 Basi, mnapofungua, huenda nikasema hili. Watu wengi husema, "Vema, je, Zaburi zina pumzi ya Mungu?" Bila shaka, zinayo. Zina pumzi.

19 Cho chote kilicho kwenye Biblia hii kina pumzi, kiwe historia, kiwe nyimbo, cho chote kile. Kimetiwa pumzi ya Mungu. Yesu alisema, "Hamkusoma alivyosema Daudi katika Zaburi?" Kisha nawaza. . . Zaburi, bila shaka, ni nyimbo. Na kama nyimbo zimetiwa pumzi na Mungu, ambazo, naamini zimetiwa, na ni za kinabii pia, natumaini nitakuwa nimesimama siku hiyo wakati huu wimbo utakapotimia.

Kutakuweko na mkutano hewani,
Wakati huo mwema, hivi karibuni;
Nitakutana nawe, na kukusalimu huko.
Kule nyumbani ng'ambo ya anga
Kuimba ambako hakujasikika, hakujasikiwa na maskio ya wanadamu,

Itakuwa yenye fahari, nawatangazieni!
Na Mwana wa Mungu Binafsi ndiye atakayekuwa Kiongozi
Kwenye ule mkutano hewani

Lo, na—nataka kuwa huko wakati huo!

20 Basi Zaburi 42.

*Kama ayala ioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu.*

*Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu, Mungu aliye hai: lini nitakapokuja nionekane mbele za Mungu.*

*Machozi yangu yamekuwa chakula changu mchana na usiku, pindi* mimi*. . .pindi wanaponiambia mchana kutwa, Yuko wapi Mungu wako?*

21 Nawaza, Daudi, kwa kuandika Zaburi hii, hapana budi alikuwa katika dhiki. Na kwa kawaida inahitaji dhiki kutoa kilicho bora sana katika mwanadamu. Ndipo, kwa kweli, hapo ndipo Mungu. . .inapofikia tunapofunga, mara nyingi, kujitayarisha kuondoa ubinafsi wetu. Na ninawaza, Daudi alipofikia mahali hapa, ndipo akaanza kutafakari juu ya Bwana, akaanza kuwazia mambo.

22 Mara nyingi, Mungu hutuingiza ha—hatarini ambapo hatuna budi kutazama juu. Mara kwa mara hatuna budi kulala chali, hospitalini ama kitandani mahali fulani, kusudi tupate kuinua macho yetu kuona ambapo baraka kuu za Mungu hutoka.

23 Sasa Neno ninalotaka kunena toka kwake usiku huu, ni neno moja kutoka katika Biblia, nalo linapatikana katika kifungu cha pili, "kiu," lile neno: *Kiu*. Nami nilitazama katika kamusi nilipokuwa nikilichunguza Neno hili.

24 Nalikuwa nikiwaza kuhusu so—somo wakati mmoja, nalihubiri juu ya *"Kuuonea Kiu Uzima."* Nami nililitoa katika Zaburi, pia, wakati Daudi aliposema, "Amri Zako," "naamini ni bora kuliko uhai."

25 Kisha nilikuwa nikichunguza na kuwazia hilo neno "kiu", basi nikaliangalia katika kamusi, kuona maana yake. Basi haya ndiyo Webster asemayo, "Ni shauku inayouma," inauma, unapotaka jambo fulani sana hata unaumwa.

26 Naam, si—si jambo lisilo la kawaida, kuona kiu. Kiu ni—ni jambo la kawaida. Ni jambo tu ambalo Mungu ametupa, tupate, kutupa sha—shauku ya kitu fulani. Wakati mwingine Mungu,

pia, amekupa m—mnara wa kusimamia, kitu fulani kilicho ndani yako, ambacho—ambacho husimamia shauku hizi mbali mbali. Na hiki kiu, M—mnara huu wa kusimamia ulio katika moyo wa mwanadamu, ni kitu ambacho Mungu alimpa ku—kumshauri juu ya shauku anazozihitaji.

27 Sasa kuna aina mbili mbalimbali za kiu. Kuna kiu, cha kimwili. Na kuna kiu, cha kiroho. Ningetaka kusoma haya, aliyosema Daudi tena.

> *Nafsi yangu* humwonea kiu *Mungu, Mungu aliye hai*. . .

28 Si ya kihistoria ama jambo lililotendeka miaka kadha iliyopita, ama—ama hadithi iliyosimuliwa na mtu fulani; bali, "ya Mungu aliye hai," Mungu aliyepo daima. Na nafsi yake ilimwonea kiu Mungu huyo, si kitu fulani cha kihistoria.

29 Sasa tunaona, Mungu hukupa mnara wa kusimamia, hukupa wewe mambo unayohitaji. Sasa, ule mnara wa kusimamia ulio ndani yako ndio unaokuongoza. Na kiu hiki huongozwa na . . . mnara, mnara wa kusimamia, ambao hukwambia unachohitaji, kunena kiroho. Mnara wa kusimamia mwilini mwako, na nafsini mwako, pia. Kuna mnara wa kusimamia mwilini mwako, ambao hukuambia haja ya mwili wako, nayo huletwa kwako na kiu. Pia, kuna mnara wa kusimamia nafsini mwako, ambao hukwambia mambo ya kiroho unayohitaji, kitu fulani rohoni mwako, na, nawe kwake waweza kujua ni uhai wa aina gani unaokuongoza.

30 Uwe—uwezapo kuona shauku zako ni nini, basi unaweza kujua, kwake, ni nini kilicho ndani yako, ambacho kinasababisha hiyo shauku uliyo nayo. Waona, kuna jambo fulani unalionea kiu, na—na linaweza kukwambia nafsini mwako shauku hii ni nini, kwa namna ya kiu ulicho nacho. Natumaini mnaweza kufahamu hayo.

31 Kuna m—mnara wa kusimamia nafsi, na mmoja wa mwili, na kila mnara hushauriana juu ya haja za mwingine. Kila mmoja huomba msaada kwa haja za mhitaji, unatuma wimbi la kutahadharisha.

32 Kwa mfano, mwi—mwili huona kiu kusudi utosheleze shauku zilizo mwilini, nayo roho huonea shauku vitu vilivyo katika nafsi, huvionea shauku, na mara nyingi hizi hupigana zenyewe. Tunaona hapo, shida ilipo siku hizi, watu wengi sana hujaribu kuishi kati ya shauku hizo mbili. Yaani, mmoja wao hutamani mambo ya duniani, yule mwingine hutamani mambo ya Mbinguni.

33 Kama Paulo alivyosema, analieleza katika Warumi 7:21, "Ninapotaka kutenda lililo jema, lipo lililo baya." Unapojaribu, je, umepata kuwa na tukio kama hilo, Wakristo? Unapojaribu kutenda jambo lifaalo, unapojitahidi kufanya jambo njema, ndipo unaona ya kwamba mna Shetani, kila upande, kukuhangaisha tu, kila kitu unachojaribu. Na hilo ndilo

jambo moja nzuri, hilo. Ningetaka kusema hili, kusudi Wakristo wajue hilo. Unapo—unapoanza kutenda jambo fulani, kuna kitu fulani kila mara kinachojaribu kukutatiza katika kulifanya, lifanye kwa vyo vyote. Huyo ni Shetani pale, akijaribu kukuzuia kufanya yaliyo mema.

34 Basi, mara nyingi, nawakuta watu ambao ni wepesi kupatwa na wasiwasi. Wanapoona kwamba wanajaribu kufanya jambo fulani, na—na kila kitu kinawazuia pande zote mbili, wao wanasema, "Huenda ikawa si mapenzi ya Bwana." Mwaona? Naam, usimwache Shetani akakudanganye hivyo.

35 Jambo la kwanza, ni kuchunguza kama ni mapenzi ya Mungu, ama sivyo. Ndiposa ukitaka kujua kama ni mapenzi ya Mungu, angalia katika Biblia. Hicho ndicho kitu kinacho—kinachokunyosha, ni Neno la Mungu; kisha ukiona liko katika Neno la Mungu, kwako kulifanya.

36 Kama, kwa mfano, kutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mara nyingi, nakutana na watu, wasemao, "Vema, nimemtafuata Roho Mtakatifu, na sikumpata. Siamini Yeye ni kwa ajili yangu. Kila mara ninapojaribu, ninakuwa mgonjwa. Ninapoanza kuomba, kama nikifunga, ninakuwa mgonjwa. Na kama nikijaribu kukesha usiku mzima, ama kuwa macho, ninashikwa na usingizi mzito. Si—siwezi kuinuka." Kumbuka, huyo ni Shetani. Kwa maana, Mungu anakutaka uwe na Roho Mtakatifu. Ni kwa ye yote atakaye.

37 Mara nyingi unaona, unapoombewa, katika mkutano, kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu, ndipo siku inayofuata unapata kwamba, bila shaka, ya kwamba Shetani ataufanya huo mbaya maradufu kuliko ulivyokuwa siku iliyotangulia. Waona? Kumbuka, huyo ni Shetani akijaribu kukuondosha kwenye baraka alizo nazo Mungu kwa ajili yako. Waona? Usisikize mtu huyo. Waona? Kila mara jitahidi kusonga mbele.

38 Nalikuwa na tukio kama hilo hivi majuzi nilipokuwa nikienda Afrika. Ikiwa nilipata kuwa na wakati ambapo Shetani alinisonga, ilikuwa kwenda Afrika wakati huu wa mwisho. Ulikuwa mmoja wa—wa mikutano mizuri sana na wakati mzuri sana ambao nimekuwa nao huko ng'ambo. Nilipata, naamini, kumaliza mambo mengi zaidi katika wakati huo mfupi nilipokuwa huko, mbali na safari yangu ya kuwinda, kuliko niliyopata kufanya wakati wo wote. Daima naliwaza ya kwamba makanisa hayo hayakunitaka kule, kisha nikagundua . . . Nilipata barua kutoka kwa mtu fulani, ya kwamba ndivyo ilivyokuwa, lo, wao hawakunitaka kule, jumuiya yote; kisha nikagundua ilikuwa mtu mmoja, mwenye barua kutoka dhehebu fulani, ambaye alisema, "Hatukutaki," alimaanisha yeye na jamaa yake. Mwaona? Kwa hivyo basi nilipofika kule . . . Mwaona, eti "sisi", hiyo ilikuwa yeye na jamaa

yake; na haikuwa hao watu, kamwe. Kwa hivyo, sasa ni uwanja mkubwa uliowekwa wazi kwa ajili yetu.

39 Mnaona, Paulo aliposema, “Ninapojaribu kutenda lililo njema, lipo lililo baya.”

40 Hebu mwongovu mpya aje usiku wa leo madhabahuni, mahali fulani hapa katika maskani haya, ama—ama kote taifani; na kumbuka tu, kesho, mama atakuwa na hasira zaidi ya alivyowahi kuwa, baba atafanya fujo, na watoto wote wa shule. Na kila kitu kinaenda mrama, kwa maana ni Shetani; akijaribu kukufanya ugeuke. Anajaribu kukuondoa Njiani. “Ninapojaribu kutenda lililo njema, basi lipo lililo baya.”

41 Basi, hebu tuchunguze kiu, na hebu tuone kama kweli kiu ni jambo la kawaida. Watu wamekuja wakaniambia, “Lo, sikufanya hilo kamwe. Naamini ni hali ya watu fulani kutaka kuwa Wakristo.” Lo, sivyo. Hilo ni kosa. Bila shaka ni jambo ambalo linamhusu kila mwanadamu. Bila shaka ni kweli. Tulipokuja humu nchini katika siku za mwanzoni, tuliwakuta Wahindi hapa. Nao Wahindi, ingawa walikuwa makafiri wakati huo, waliabudu jua ama cho chote kile. Mradi tu wao ni wanadamu, kuna kitu ndani yao, kiu ya maumbile, inayomlilia Mungu, mahali fulani.

42 Kule mwituni, hivi majuzi kule nyuma, maili mia nne na themanini nje ya ustaarabu ulio karibu sana, mji mdogo sana wenye yapata watu elfu tatu, wa Beira . . . kule Mozambique. Tuliwaona wenyeji ambao hata . . . hawakupata kumwona mzungu. Nalimwona msichana wa kienyeji, hakuwa amevalia nguo, (ni vigumu kumwona aliyevalia nguo), naye alikuwa ameketi juu ya mti. Nami nilikuwa nikimfuatilia simba, na kulikuwa . . . nikasikia kitu kama mwanadamu, akipiga mayowe. Huyu msichana wa kienyeji ameketi juu pale, amekodoa macho, huku amemshika mtoto mchanga. Naye alichokuwa anaogopa . . . Hiyo ndiyo kinga yake pekee, ni kupanda mtini, kutoka kwa simba, chui ama cho chote kile, ama mnyama fulani. Naye alikuwa ameniona, na kusikia ilikuwa mwanadamu, bali alipotazama na kumwona mzungu! Hakuwa amemwona ye yote maishani mwake, mwaona, naye aliogopa nusura afe. Mwaona?

43 Bali tunapowaona watu hao, hata katika hali hiyo ya kishenzi kule, walikuwa wangali wakiabudu. Kabla ya kumpata simba, wao walimwaga ugali (huo ndio wanaokula) juu ya jani dogo, na kupiga makofi, na kuita roho fulani wa kitu fulani kikuu hawakujua kiko wapi (kama alivyo mtakatifu mlinzi ama cho chote kile, kwa Mkatoliki), kuwakinga, kusudi wasiuawe wakati huyu simba anapowavamia.

44 Mnaona, ni kitu cha maumbile. Si jambo lisilo la kawaida kumwonea kiu Mungu. Ni jambo la kawaida. Ni jambo tu likupasalo kutenda. Mungu amekuumba hivyo. Na si mtu

maalum, bila shaka ni mtu wa kawaida. Si ati ni jambo maalum kwa watu fulani.

45 Wao husema, “Vema, nimeona watu fulani wakiishi ma—maisha ya ushindi sana, hata wao daima wako juu ya nyumba, wakimsifu Mungu. Laiti ningalijisikia hivyo.” Vema, sababu ya kujisikia hivyo, ni kiu kilicho ndani yako. Na hicho ni kitu cha kawaida. Ni kwa kila mtu, kumwonea kiu Mungu.

46 Sasa, tutachukua kiu cha kawaida kwanza. Hebu tuchukue, kwa mfano, kiu cha maji. Kama alivyosema Daudi hapa, kuona kiu, cha “maji.” Kiu cha maji, mwili unahitaji maji. Na kama hutoshelezi kiu hicho, utaangamia. Utaishiwa na maji, na hu—hutaishi. Kama hauwezi kupata maji kwa, hicho kiu, kutuliza hicho kiu cha mwili wa kawaida utakufa punde tu. Hautaishi kwa muda mrefu. Unaweza kuishi muda mrefu zaidi bila chakula kuliko unavyoweza kuishi bila maji. Maana, unaweza kufunga kwa siku arobaini. (Yesu alifanya hivyo), nadhani, bila—bila chakula, bali hungalidumu muda huo bila maji. Ungekauka tu na kufa. Huna budi kupata maji. Na—na kiu unachokipata, naam, ni kuonyesha ya kwamba mwili unahitaji kitu fulani, kuishi. Mwili hauna budi kupata maji, kusudi uendelee kuishi. Wewe ni asilimia themanini na kitu maji na petroli, kwa vyo vyote, na huna budi kuingiza vitu hivi, upate kuwa hai. Kama nilivyosema, ukizipuuza utaangamia.

47 Kiu pia ni kengele. Ni saa yenye kengele, huko kuona kiu. Nafsi hupiga kengele ya saa, kijikengele kilicho ndani yako kinachokwambia ya kwamba mauti yanaotea hapo karibu. Ya kwamba, usipopata maji upesi sana, huna budi kufa. Nayo huzidi kutoa sauti kubwa, hata hatimaye ukiendelea kuinyamazisha utakufa, kwa sababu ni saa yenye kengele.

48 Kama Daudi alivyoieleza hapa katika Zaburi, “Kama ayala aoneavyo shauku mito ya maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu.” Kama ayala aoneavyo shauku mto wa maji!

49 Mara nyingi nimefikiria, ninaposoma habari hizi za Daudi. Daudi alikuwa mtu wa mwituni, mwindaji. Naye aliwinda kulungu, bila shaka. Na wengi wetu, siku hizi, huwawinda. Na ayala ni kulungu.

50 Nasi tunaona, kama umewaona mbwa, mbwa mwitu watamshika kulungu. Na mara nyingi wao wana chonge, kama yule mbwa mwitu mdogo. Naye anaweza kumshika kulungu kwa ghafla karibu na sikio *hapa*, na kuuning’inisha uzito wake. Yeye analikata koo la huyo kulungu, naye kulungu huyo hawezi kupona basi. Bali wakati mwingine huyo m—m—mbwa, kama kule Afrika, mbwa mwitu atamshika kulungu ubavuni, akilikosa koo. Atamshika, mara ya pili, ubavuni. Na iwapo huyo kulungu ana nguvu kutosha ama ni mwepesi kutosha, anaweza kumtupilia huyo mbwa mbali.

51 Kulungu yuna mbio zaidi. Mbwa humnyemelea wakati haangalii, na wakati upepo haumwelekei, na—naye—naye hajui m—mbwa yu karibu.

52 Ndiposa mbwa mwitu anapomshika, iwapo yeye ni mwepesi sana, anaweza kumtupilia mbali. Na, lakini huyo mbwa anapotoka ubavuni, ana kipande kizima cha nyama ya kulungu mdomoni mwake. Ama, anapomkamata shingoni wakati mwingine, yeye atamrarua karibu na mshipa mkubwa wa shingoni, na kuukosa. Naye huyo kulungu, akimtikisa, atakirarua kipande kikubwa cha nyama toka shingoni mwa huyo kulungu, kisha damu inaanza kutiririka.

53 Ndiposa huyo mbwa ataifuatilia hiyo damu, akimfuata huyo kulungu. Na uhai wa kulungu unapoanza kufifia, na kama hiyo damu, ndiyo uhai wa mwili, hiyo inapoanza kufifia, naye kulungu anaaza kuwa mdhaifu. Na yule mbwa basi, ama mbwa mwitu, yu papo hapo nyuma ya huyo kulungu.

54 Sasa, kama huyo kulungu hawezi kupata maji! Naam, maji yana kitu ndani yake, ambacho, kulungu anapokunywa maji hayo, yanakomesha kutokuwa na damu. Bali asipopata maji kumbaridisha, basi da—damu inaendelea kutoka zaidi; kwa maana yeye anakimbia, huku moyo wake unapiga. Walakini kama angalipata maji tu, huyo kulungu ataishi.

55 Sasa, kuna somo kuu hapo, mnaona, na Daudi akisema hapa, "Kama ayala ioneavyo shauku mto wa maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu."

56 Basi huyo kulungu anajua, asipopata maji amekwisha. Hawezi kuishi kamwe. Nimewafuatilia mara nyingi baada ya kujeruhiwa. Anapofikia kijito cha maji, yeye atakivuka na kunywa maji, apande upande wa juu; ashuke chini, avuke, anywe maji na apande upande wa juu. Hauwezi ukamshika, mradi tu atakifuatilia hicho kijito. Bali mara anapokiacha hicho kijito, iwapo hawezi kupata kijito kingine mahali fulani, utampata tu. Naye kulungu anajua hivyo, kwa hivyo atakaa karibu tu na maji, anapoweza kuyafikia upesi sana. Je, ungaliwazia kulungu aliyeinua pua lake, amenaswa mahali ambapo Namna maji?

57 Naye anasema, "Kama ayala inavyoonea kiu ama ioneavyo shauku ni kia mito ya maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu. Nisipokupata Wewe, Bwana, nitaangamia. Si—si—siwezi kwenda isipokuwa nikupate!" Na wakati mwanamume, au mwanamke mvulana ama msichana, anapopata kiu cha namna hiyo kwa ajili ya Mungu, atapata kitu. Mwaona?

58 Bali tunapoiendea, nusu-nusu tu, "Vema nitapiga magoti nione atakayofanya Bwana." Mwaona, hamwoni kiu bado. Inapaswa kuwa kiu cha mauti na Uzima, ndiposa jambo fulani litatendeka.

59 Kulungu, pia hapa yeye ni. . .Tunaona ya kwamba yeye pia ana hisi nyingine, ya kunusia, ambayo hupiga kengele ndani yake adui wake anapomkaribia. Yeye a—ana, maskini kiumbe hiki, kina hi—hisi ya kujilinda chenyewe. Naye a—ana kijikengele ndani yake, kitu fulani kidogo, ambacho hugutusha pua lake adui anapokaribia. Unaweza kuwa katika upepo wa adui, naye anajua uko, pale, na aende zake. Wakati mwingine umbali wa nusu maili, yeye anaweza kukunusa na kutoroka, au mbwa mwitu au hatari yo yote. Anaweza kuihisi kwa sababu yeye ameumbwa hivyo. Yeye ni kulungu, asili yake. Na hisi hiyo iliyo ndani yake ni moja tu ambayo Mungu aliyompa, kumhisia, apate kuishi kwayo.

60 Nami nalidhani, nikilinganisha kulungu na mtu anayemwonea kiu Mungu, kabla adui hajamfikia. Kuna jambo fulani kuhusu mwana wa Mungu, ya kwamba mara unapozaliwa katika Roho wa Mungu, unapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuna kitu fulani kuhusu mtu huyo kinachoweza kumhisi adui. Unaweza kumchukua mtu anapochukua Maandiko, na kusoma Maandiko na kujaribu kuingiza kitu fulani kwenye hayo Maandiko, kinachopinga Maandiko, mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu anaweza [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] kuhisi hilo, upesi sana. Kuna kitu fulani kigeni. Anapofikia mahali fulani, na—na hiyo hisi fulani dogo mle, imeumbwa kuyalinda maisha yako. Wewe, usithubutu, usithubutu kukiendea cho chote isipokuwa ni Neno la Mungu hasa. Inakupasa kudumu na hilo Neno hasa. Na, sasa, nasi tuko salama kwa hiyo hisi mradi tu tumo katika Roho Mtakatifu.

61 Unaweza kuanza kusoma, na kama kwa mfano, mtu fulani aseme, nami naenda kusoma katika Marko 16, na kusema, "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya, ama watashika nyoka, ama wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

62 Sasa basi, unamwona mtu akisimama pale na kusema, "Naam, hayo yalikuwa ya wakati wa kimitume." Hiyo, sasa, upesi sana, kama umempokea Roho Mtakatifu, umekabidhiwa hiyo hisi. Inaanza kazi. Mna walakin pale. Waona? Wanajaribu kuyaeleza vingine, ya kwamba ni ya wakati mwingine, ya kwamba kweli huhitaji mambo hayo siku hizi. Bali Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Waona, mna kitu kidogo kinachoanza kutenda ndani yako, kijikengele, kwa kujua ya kwamba hilo ni kosa na hiyo ni njia ya mauti.

63 Maana, Yesu alisema, "Tukiongeza neno moja kwa Hiki, ama kuondoa Neno moja Kwake, sehemu yetu itaondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Mnaona, si Andiko moja. Inatupasa kulichukua tu jinsi lilivyoandikwa. Naye Mungu huchunga Neno Lake, kulitekeleza, nasi tunajua ya kwamba halina budi kuwa sahihi kabisa.

64 Kwa hivyo basi, haidhuru kanisa litasema nini, kile mtu ye yote yule angalisema, kama umezaliwa kwa Roho wa Mungu, unakuwa sehemu ya Biblia. Mungu alimwambia Ezekieli, alikuwa nabii, Yeye alisema, "Litwae gombo na ulile," ndipo huyo nabii na lile gombo wakawa kitu kimoja. Na huyo ni mwamini anapompokea Roho Mtakatifu; Roho Mtakatifu aliandika Biblia, na Roho wa Mungu ndiye Neno la Mungu. "Maneno yangu ni Roho. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Na unapokuwa sehemu ya hilo Neno, lo, basi hebu kitu fulani kitokee kinyume cha hilo Neno, [Ndugu Branham anadata kidole chake mara nyingi—Mh.] kuna kijikengele kinacholia upesi sana. Waona, kinakuonya ya kwamba mauti yako njiani. Haitupasi kufanya hivyo kamwe. Pia kuna . . .

65 Kiu hizi ni za kawaida tu. Ni za kawaida kwa Mkristo. Ni za kawaida kwa mwanadamu.

66 Kuna kiu pia cha kufaulu. Watu wengi sana siku hizi, jinsi tunavyoenda shuleni kwa ajili ya kiu! Tuliona, walianzisha chuo kikuu. Nasi tunaenda kule, na watu wanatumia maelfu ya dolla kuwatuma watoto wao shuleni, na—na kwenye vyuo vikuu na vyuoni, na kadhalika, kupata elimu, "Kufaulu," wanakuita, "maishani." Lakini sasa sina upinzani juu ya hilo, sasa, hiyo ni sawa. Bali, kwangu, ungalipata elimu yote duniani na bado haujapata kufaulu kunakofaa. Hiyo ni kweli. Kwa maana, hiyo itarahisisha mambo kidogo kwako hapa. Na kuna . . . Bali utakapokufa, utaacha hayo yote nyuma, na huu uchumi wote tulio nao.

67 Nilikuwa nikisema hivyo hivi majuzi, kule Phoenix. Inastahili kunukuliwa tena, ya kwamba, "Ustaarabu huu wote wa kisasa, mpango wote wa elimu, mpango wote wa kisayansi, ni kinyume cha Neno la Mungu na mapenzi Yake." Ustaarabu bila shaka ni . . . Hakutakuwepo tena na ustaarabu katika ulimwengu ujao, kama huu. Huu ni ustaarabu uliopotoshwa. Mungu alikuwa na ustaarabu Wake wa kwanza duniani, aliposema Maneno Yake na zikachipuka, kila mbegu kwa jinsi yake, na katika ustaraarabu huo hapakuwepo mauti, ugonjwa, huzuni. Na sasa tunachukua vitu vilivyo katika ulimwengu huu wa sayansi, vilivyowekwa humu kuushikilia, na kuvipotosha vinginevyo, na hiyo husababisha mauti.

68 Kama bomu la atomiki. Sijui utaratibu wa mambo haya, bali huenda nikasema hili makosa. Wao huchukua madini ya uranium, kuvunja vi—vitu vidogo sana, navyo vitu hivyo huvunjwa vikawa atomi. Inafanyaje basi? Inaangamiza, karibu, huangamiza tu. Kila kitu tufanyacho!

69 Tunachukua madawa, tunachanganya kipimo *hiki* na kipimo *hiki,* kutibu *huu*, na kuinywa. Nasi tunafanyaje? Tunararua kitu kingine.

70 Basi nadhani mmesoma, mlisoma gazeti la Reader's Digest, la mwezi uliopita, lililosema ya kwamba, "Katika wakati huu tunamoishi sasa, kwamba, vijana waume kwa wake wanafikia umri wa makamu kati ya umri wa miaka ishirini na ishirini na mitano." Wazia hilo. Wasichana wadogo wanaingia ugumba, wakiwa na umri wa miaka ishirini, ishirini na mwili na ishirini na mitatu, watu wa makamu. Mnaona nini kilichosababisha hilo, ni chakula cha mbegu zilizochanganywa na vitu tunavyokula. Mnaona, ni vitu hivyo, chakula na—na maisha tunayoishi. Wanasayansi wametuletea hayo, na, kwa kufanya hivyo, wanawaua.

71 Nilikuwa kule Afrika nilikoona hao wavulana ambao hawajakunywa dawa yo yote maishani mwao. Wanakula nyama zilizojaa mabuu. Wanakunywa maji ya kidimbwi yanayoonekana kana kwamba yangalimuua fahali. Nami nilikuwa nikipiga shabaha umbali wa yadi mia mbili, nami singaliona kwa darubini ya saba-hamsini. Na mtu mmoja wa umri wangu alikuwa amesimama pale, akiniambia ilipolenga kwa kuona kwa macho yake. Naam, kama ustaarabu huu wote wa kisasa umefanya jambo fulani. . . Naona kama nilikuwa na macho yake na tumbo lake, ningalikuwa bado mtu mzuri sana. Naam.

72 Basi mwaona, hivyo ndivyo sayansi, elimu, ustaarabu, vinavyotuangamiza. Tunajiangamiza wenyewe. Ilianza katika bustani la Edeni, na inaendelea hata wa leo. Bali, tukionea kiu ufanisi!

Kisha, tunaonea kiu ushirika. Tunaenda, tunataka ushirika.

73 Ni kama kijana mwanamume au kijana mwanamke. Basi, si jambo lisilo la lazima ama si (namaanisha) jambo lisilo la kawaida kwa kijana mwanamume na kijana mwanamke ku—kupendana wao kwa wao. Ni kiu ya mapenzi. Ni wakati wao, na wao—wao wanapendana. Na si jambo lisilo la kawaida, hilo ni jambo tu la kawaida kwao kufanya hivyo.

74 Sasa tunaona mambo mengi, katika maisha tunayoishi katika mwili wa kawaida, ambayo tunayaonea kiu. Ni kitu tu kilicho ndani yetu. Tunataka kukifanya, tunajisikia kabisa ya kwamba ni cha lazima. Na ni lazima tukifanye.

75 Sasa tunaona wanawake wengi, katika siku hizi, wanaonea kiu urembo. Naam, hamna mwanamke. . . Ni jambo la kawaida kwa mwanamke kuonea kiu kuwa mrembo. Hiyo—hiyo ni tabia aliyopewa na Mungu na—na urembo wake aliopewa na Mungu kwa ajili ya mumewe. Na sasa tunaona ya kwamba wanawake wanataka kuwa hivyo. Ni kwa nini? Ni kwa sababu ni kitu

alichopewa na Mungu. Na si vibaya kwa wanawake kuwa warembo. Inawapasa kuwa hivyo.

76 Pia, wajua, wao ndio viumbe tu ambao wa kike ni warembo kuliko wa kiume, iko katika wanadamu. Mnyama mwingine wo wote, chukua ng'o—ng'ombe na fahali, kulungu wa kike na wa kiume, kuku na jimbi, mama ndege na baba ndege, daima utaona ya kwamba wa kiume ni mkubwa zaidi na mrembo pia. Bali kwa wanadamu, inaonyesha hapo ndipo upotovu ulipopitia, inabadilika; na ni wanawake basi walio—walio warembo, nao wanatamani kuwa warembo.

77 Si kama viumbe wa kishetani tuwaonao barabarani za siku hizi; la, la, si urembo wa aina hiyo. La. Hicho ni kitu cha kuchukiza sana nilichoona maishani mwangu. Naam, bwana. Huo ni upotovu unaopotosha kiu cha kweli.

78 Naam, kiu cha kweli mwanamke anachopaswa kuwa nacho, ni "kujipamba kwa mavazi ya kujisitiri, na kuwa na roho inayofanana na ya Kristo," I Timotheo 2:9. Basi hivyo ndivyo inampasa mwanamke kutaka sana kuwa. Naam, ukitaka kuwa mrembo, hiyo ndiyo njia inayokufanya mrembo, unaona, ni roho inayofanana na ya Kristo, na kujipamba kwa mavazi ya kujisitiri.

79 Lo, jamani, baadhi ya hawa watu siku hizi barabarani! Hauwezi kutofautisha mwanamume na mwanamke, na ni—ni kitu cha kuchukiza sana ambacho wewe. . . Mimi, ni—ni . . . si—sijaona kitu kama hicho, kama mwanadamu. Imezidi binadamu. Macho yaliyopakwa rangi kote *hivyo*, na, mwajua, hayo macho ya kigeni ya mjusi, na hizo nguo zote hizo zinazoonekana ajabu. Basi, mbona, hata hazina . . . Wote hawana umbo, kabisa, hata hawaonekani kama binadamu. Na baadhi yao wavulana huku, nywele zao zimechanuliwa nyuma, mikunjo ya dada zao hapa, mwajua, kwa nini, ni upotovu mkamilifu! Hiyo ni kweli. Ni—ni—ni Shetani, na Shetani ni mpotoshaji.

80 Mungu alipofanya kila kitu katika bustani ya Edeni, kilikuwa kizuri, kisha Shetani akaviingilia na kupotosha. Shetani hawezi kuumba cho chote. Kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu. Bali Shetani hupotosha uumbaji wa asili. Na sasa ameanza (haya nataka kuyanena usiku wa leo) kupotosha ki—kiu cha asili.

81 Sasa, mwanamke, kama nilivyosema hapo awali, anataka kuwa mrembo. Kuna kitu ndani yake, ya kwamba yeye ni wa kike naye anataka kuwa hivyo.

82 Bali jinsi walivyo barabarani siku hizi, wamenyolewa kama wanaume, wamevalia nguo za mwanamume, naye mwanaume amegeuka, amevalia nguo za wanawake, kunyolewa nywele kama mwanamke. Mwaona ni upotovu, jambo lote! Chakula chenu kimepotoshwa. Maisha yenu yamepotoshwa. Kiu chenu kimepotoshwa. Shauku zenu zimepotoshwa. Ni siku za upotovu!

83 Nalikuwa nikinena hapa, si muda mrefu uliopita, juu ya *Edeni ya Shetani*. Mungu alichukua miaka elfu sita, akafanya Edeni kamilifu. Shetani akashuka na kuzinyunyizia mbegu, na kuziharibu. Sasa amekuwa na miaka elfu sita, naye ana Edeni yake ya kisayansi, kurudia tena katika upotovu wa kilicho halisi.

84 Na huu ni wakati wa kuchanganya mbegu, kuchanganya mbegu. Wao hata wana ma—makanisa siku hizi, yangali mchanganyo. Hiyo ni kweli. Wanaingia humu, wanaenda tu kanisani, ni nyumba ya kupangisha badala ya kanisa. Kanisa ni mahali ambapo watu huja kumwabudu Mungu katika Roho na Kweli. Na siku hizi ni nyumba ya kupangisha. Tunaenda kule na kuwa na wakati mdogo wa kusalimiana kwa mikono, na kushirikiana, na kahawa kavu nyuma ya jengo, kisha tunaenda makwetu hadi juma lijalo, nasi tumetimiza wajibu wetu wa kidini.

85 Basi ni wakati uliopotoshwa. Na Shetani anapotosha kiu hizi ambazo Mungu aliziweka ndani yenu, kuonea kiu. Shetani anazipotosha. Sasa ukitaka kuona yaliyo kweli, upotovu . . .

86 Kama ninyi, wanawake, mkitaka kuwa warembo, chukueni I Timotheo 2:9, ambayo ni "kujipamba wenyewe katika mavazi ya kujisitiri—mavazi, pamoja na roho kama ya Kristo, iliyo pole, wakiwatii bwana zao," na kadhalika. Hivyo ndivyo iwapasavyo kujipamba, maisha mnayoishi.

87 Yeye anapotosha tabia ya kweli ya Mungu, na kiu halisi cha Mungu, cha mwili na nafsi, kwa tamaa ya dhambi. Dhambi, upotovu! Sasa, tunaona ya kwamba, mtu siku hizi, jinsi walivyouchukua huo upotovu; kiu cha Mungu, kiu cha kuwa warembo, na viu hivi vyote. Cha, cha maji, wamegeuza hicho kwa kukiridhisha kwa pombe. Kiu cha furaha, kila mtu anataka kupata furaha; kiu cha ushirika; hivi viu vyote ambavyo Mungu huweka ndani yetu, kusudi tupate kumwonea kiu. Mungu alikuumba upate kumwonea kiu, nasi tunajaribu kuridhisha hicho kwa kiu cha namna nyingine, kwa upotovu wa aina fulani nyingine ya kiu halisi. Mnaona jinsi ilivyo katika mambo ya kawaida? Mnaona ilivyo katika mambo ya rohoni? Tunawaza, mradi tu tunajiunga na kanisa, hilo—hilo linatosha, hivyo ndivyo tu itupasavyo kufanya. Vema, hilo ni kosa kabisa. Sivyo.

88 Mungu anakutaka umwonee kiu! "Kama ayala iuoneavyo shauku mto wa maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu." Mnaona, mnaona?

89 Basi, kama huyo kulungu alikuwa akiuonea shauku mto wa maji, vipi kama mtu angalikuja, na kulungu mwenziwe angalikuja, na kusema, "Aisee, nitakwambia ni—nitakalofanya. Najua palipo shimo la matope huku." Vema, kulungu hangalitaka hilo. Hilo halingalimfaa yeye kitu.

90 Na hamna kinachoweza kuridhisha hiyo shauku iliyo ndani ya mwanadamu, hata Mungu anapoingia ndani. Hana budi kuipata, ama afe. Na hamna mtu anaye haki ya kutuliza ama kuridhisha hiyo shauku takatifu, iliyo ndani yake, kwa mambo ya ulimwengu. La, bwana. Ni kinyune cha Mungu kufanya hivyo. Na kama unamwonea Mungu shauku, usisalimiane kwa mikono na mhubiri na kuandika jina lako katika kitabu. Kama unamwaonea Mungu shauku, kuna jambo moja tu la kuiridhisha, hiyo ni, kukutana na Mungu. Kama unamwonea Mungu shauku, hivyo ndivyo tu unavyoweza kukutana Naye, ni kufanya hivyo.

91 Kisha kuna hatari kubwa, pia, kama huangalii unayofanya wakati huo. Kama una shauku ya Mungu, hakikisha ni Mungu unayempata. Waona, hakikisha ni shauku yako inayoridhishwa. Lakini kama Shetani amefaulu kukupotosha, kutoka hizi tamaa za maumbile, na atafanya hayo akiweza, ata—atakufanya tu ujaribu kuridhika.

92 Mtu anatoka nje, nini kinachomfanya mtu kulewa? Ni kwa sababu ana mashaka na wasiwasi. Ana kasoro.

93 Nalikuwa kwa Mayo, hapa si muda mrefu uliopita, nami nilikuwa kule kwa mahojiano. Kisha ikasemwa eti, ya kwamba, wakinena kuhusu unywaji, nami nikawaambia ya kwamba baba yangu hunywa pombe.

Kasema, "Nini kilimfanya kunywa?"

Nikasema, "Sijui."

94 Yeye akasema, "Ni kwa sababu kuna kitu ambacho (yeye) hakikumridhisha, naye akawaza angalikunywa kukiondolea mbali mawazoni mwake."

95 Nikaipata papo hapo, waona. Ilikuwa kweli Mungu ndiye kitu pekee kinachoweza kuridhisha hiyo shauku. Mungu mwenyewe ndiye kitu pekee kinachoweza kuridhisha hiyo shauku ya mwanadamu, ni kumkubali Mungu.

96 Basi Shetani huchukua vitu hivi, kama nilivyosema, na kuvipotosha. Kisha kama wewe—kama wewe. . . Kama hutaipa hiyo shauku mahali panapofaa maishani mwako, nawe hutaona shauku na kuchukua vitu ambavyo Mungu alitoa kutuliza hiyo shauku kwake, kuikomesha, basi Shetani atakuongoza kwenye shimo lake la maji machafu ya ulimwengu huu. Huna budi kuyapata mahali fulani. Kama hauwezi kupata chakula, unaweza kula kutoka pipa la taka. Waona? Na kama—kama hungalipata maji, nawe ulikuwa wafa, ungalikunywa toka ki—kidimbwi cha namna yo yote, kwa maana unaangamia.

97 Bali hamna sababu ya hiyo, unapomwonea Mungu shauku, kwa maana Mungu ni Mungu aliye hai, si kitu cha kihistoria. "Nafsi yangu hukuonea shauku, Wewe, Mungu uliye hai," Kitu ambacho hutoa maji yaliyo hai, kitu kinachoridhisha.

98 Kuna asili nyingine, ya kawaida, shauku ya asili, katika hiyo shauku ya nafsi. Huenda ukasema, “Ndugu Branham, je, hiyo shauku ya nafsi, hiyo ni ya kawaida?” Naam, ni kawaida kwa nafsi kuona shauku. Nayo ni, kwa maana Mungu alikuumba hivi, ili upate kumwonea shauku. Yeye anakutaka umwonee shauku. Naam, Mungu alikuumba hivyo. Haikumlazimu kukuumba hivyo, bali alifanya hivyo. Na kama hangalikuumba hivyo, kusudi upate kuona shauku, kungalikuwa na udhuru kwenye ile baraza ya Hukumu, tasema, “Si—si—sikumwonea shauku Mungu kamwe.” Bali, hamna udhuru, unamwonea shauku. Utaifanya vinginevyo; huenda ukaifanya mke wako, huenda ukaifanya motokaa yako, huenda ukaifanya kitu kingine, huenda ukaenda kanisani na kujaribu kuiridhisha. Nami sina neno juu ya kwenda kanisani, bali hiyo si uradhi. Ni kumpata Mungu, Mungu aliye hai, Mungu wa Mbinguni, nafsini mwako, ambaye huridhisha shauku hiyo kubwa uliyonayo, sasa.

99 Maana, Yeye alikuumba upate kumwonea shauku, kwa ajili ya ushirika. Naam, kuna shauku halisi ya ushirika. Sasa sisi hupenda kukutana sisi kwa sisi. Tunafanya hivyo usiku wa leo. Tumekutanika hapa usiku wa leo kwa sababu sisi hupenda kushirikiana, sisi kwa sisi. Mbona tunafanya hivyo? Kwa maana kuna kitu ndani yetu kinachotufanya tuwe na hamu ya kukutana. Hilo ni jambo la kawaida. Na sasa tunakutanika kwa hali moja hapa, hiyo ni, kwa sababu sote tuna shauku ya Mungu. Mnaona? Ndiposa tunakutanika hapa katika hali hii ya kawaida hapa kwa ushirika. Kanisani usiku wa leo, hapa, huenda kukawa na mawazo mengi ya kidhehebu, na kadhalika; bali ifikiapo hicho kiu, tunaweza kukutana katika hali moja, mahali pamoja: sote twaona shauku. Wengine huenda wanaamini katika kunyunyizia, wengine katika ubatizo, mwingine katika kumwagilia, na kadhalika; bali ifikiapo ile shauku ya Mungu, tuna—tunakuja kwa hali moja. Naye Mungu alituumba tupate kufanya hivyo, kumwonea shauku na kuwa na hamu ya ushirika Wake. Sijui cho chote . . .

100 Nilipokuwa mvulana mdogo, nakumbuka nililelewa katika jamaa maskini sana. Nami nakumbuka wakati mwingi ningeenda kutembea na watu. Singelivalia inavyostahili ukienda mahali pa maana. Bali, si—sijui, kuna jambo fulani kuwahusu watu, ambalo nalipenda. Nilipenda kuambatana nao. Bali nilikuwa, kwa kadiri, kile kinachoitwa, kondoo mweusi. Na nilipookoka na kupata Kitu hicho ndani yangu, nilichokionea shauku, Ra—Rafiki, Mtu ambaye angekuwa rafiki msiri wangu, Mtu ambaye ningalimwamini, Mtu ungaliketi naye na kuzungumza shida zako naye. Na wakati . . . Nalipata uradhi halisi na wa kweli nilipompata Yesu Kristo, yule Mridhishaji wa kweli aniondoleaye yote—yote . . . atulizaye shauku hiyo yote, na akupaye kitu ambacho—ambacho inaonekana kama hamna kitu kinachoweza kuchukua mahali Pake.

101 Na sasa jinsi Shetani hujaribu kupotosha huu uradhi wa nafsi, ile shauku ya nafsi! Yeye hujaribu kukupa kila kitu kuiridhisha. Naye ni wa uongo sana katika siku hizi za upotovu. Huu ni ulimwengu uliopotoshwa. Ni jamii iliyopotoshwa. Ni watu waliopotoka. Kila kitu kimepotoshwa, na imepotoshwa pole pole sana hata umekuwa wakati wa udanganyifu sana mwanadamu ye yote aliopata kuishi ndani yake. Ni wa udanganyifu sana kuliko ulivyopata kuwa.

102 Sasa huwezi kamwe—huwezi kamwe kuwazia jinsi taifa limekuwa lenye hila, hata kwa ndugu zetu wenyewe, kama watu wa Amerika.

103 Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi. Nilikuwa mwituni majuma machache yaliyopita na kupata pa—pa—pakiti ya sigara mwituni. Nayo ilisema pale, "Chujio la mtu mwenye busara." Kisha nikaingia mwituni kidogo, kisha nikarudi; nikazidi kuwazia mawazoni mwangu, "Chujio la mtu mwenye busara, na ladha ya mvutaji wa sigara."

104 Vema, nalikuwa kwenye Maonyesho ya Ulimwengu, miaka kadhaa iliyopita, kumbuka walikuwa na yule Yul Brynner na wengine kote kule, walipokuwa wakionyesha maonyesho ya sigara. Na jinsi walivyochukua huo moshi na kuupulizia kwenye kipande cha marmar, na kuiparuza hiyo sumu ya sigara toka pale, na kuiweka mgongoni mwa panya. Katika muda wa siku saba, huyo alikuwa amejaa kansa sana hata hangalisimama kwa miguu yake. Mnaona, kutoka kwa sigara moja! Kisha wakaonyesha mambo yalivyo hiyo iingiapo katika mapafu ya binadamu. Wengine wao husema, "Sivuti. Mimi huipulizia midomoni mwangu." Inaonyesha jinsi inavyoingia katika mate na kuingia ndani vile vile, kupitia kooni, mwaona.

105 Naye huyu mtu akasema, "Mmeona maongezi mengi kuhusu chujio." Akasema, "Sasa, kama ukiwa na tamaa," kukiweko shauku, waona, "tamaa ya kuvuta sigara, sigara moja ya kawaida huenda ikaridhisha hiyo tamaa wakati uliopo. Bali ukiwa na chujio, inachukua sigara nne kuridhisha," kasema, "kwa sababu unapata tu theluthi moja tu ya moshi."

106 Naye kasema, "Ladha ya mvuta sigara?" Waona huwezi kupata moshi usipopata lami. Nawe upatapo lami, una kansa. Ni hivyo basi, waona, ni—ni hila tu. Nami nawazia kampuni ya—ya sigara iliyo humu nchini, na—na hutegemea taifa hili, na basi iwe na hila kama hiyo, kuwadanganya kabisa wananchi wa Amerika, kuwadanganya. Chujio ya mtu mwenye busara? Ni hila tu za kuuza sigara zaidi.

107 Kisha nikawazia kitu hicho, "Chujio la mtu mwenye busara," nikawaza, "hilo ni wazo nzuri." Kwa hivyo kuna Chujio la mtu mwenye busara, hiyo ni Biblia hii. Chu—chujio la mtu mwenye busara itachukua Chujio hili. Italeta ladha ya mtu mwenye haki. Waona?

108 Naam, huwezi kupitishia dhambi katika kurasa za Biblia hii. La, inazikomesha. Inaichujia nje. Sasa, unaweza kwenda kanisani, na uchukue cho chote, bali hauwezi kupitia katika Biblia hii na uwe na dhambi. Haiwezekani. Inazichuja dhambi zote, na inatoa ladha ya mtu mtakatifu. Kwa sababu kama mtu anafikiria ya kwamba anataka kuwa mtakatifu, na kuwa kama Mungu, na kuwa mwana ama binti wa Mungu, basi anahitaji chujio linalofaa. Kwa hivyo anaacha dhambi zote upande huu wa Biblia, naye anaweza kupitisha tu Roho Mtakatifu katika Biblia, aliyeiandika Biblia. Ni ladha ya mtu mtakatifu, kuwa na Chujio hili la mtu mwenye busara.

109 Sasa tunaona jinsi kulivyo na udanganyifu siku hizi. Mathayo 24:24, Yesu alisema, "Katika siku za mwisho, ya kwamba, zile roho mbili zitafanana sana hata zingewadanganya, hata walio Wateule kama yamkini." Jinsi zinavyofanana! Jinsi ulivyo udanganyifu wa—wa ukweli na uongo tulio nao siku hizi!

110 Hata katika serikali ye—yetu, katika siasa zetu, ha—hatuna hata na mtu tunayeweza kumchagua kama mwanasiasa, ambaye atasimama kabisa na yale anayofikiri ni ya haki. Wako wapi akina Patrick Henry na akina George Washington, na akina Ibrahim Lincoln wetu wa siku hizi? Kama tu Rais wetu alivyosema pale, "Njia ni, wakitaka ukomunisti, wanaweza kuupata, cho chote wanachotaka watu." Iwapo hiyo si m—mtu ambaye hatanena anayosadiki. Mwanaume atakayesimama na kanuni zake atakayesimama na kile kilicho kununi . . . anataka tu kuendea nji—nji—njia isiyo na pingamizi.

111 Na hivyo ndivyo watu wamekuwa, kanisani. Wanataka kuja kujiunga na kanisa, nao husema, "Lo, vema, ba—basi, ni—nimejiunga na kanisa sasa." Unajaribu kuridhisha hiyo shauku kuu takatifu ambayo Mungu aliiweka ndani yako, huo Mnara wa kusimamia unaojaribu kukuelekeza kwa jambo lililo njema, nawe unajaribu kuiridhisha kwa kujiunga na kanisa, kunukuu kanuni za imani, ama kitu kama hicho. Ambapo, si kitu kingine ila ni Uwepo wenyewe na kujawa na Mungu mwenyewe maishani mwako, ambako kutaridhisha huyo.

112 Yeye hataridhishwa kwa kanuni za imani. Hauwezi kamwe kupitisha kanuni za imani katika Biblia. La. Hakuna inayodhaniwa kuwa Imani ya Mitume, itakayopitia mle kamwe. Nionyeshe katika Biblia ambapo Imani ya Mitume husema, "Naamini katika kanisa Takatifu Katoliki la Kirumi; naamini ushirika wa watakatifu"; na huku Biblia ilisema, "Kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, na huyo ni Mwanadamu Kristo Yesu." Hautaweza kamwe kupitisha hayo katika Biblia.

113 Hutaweza kamwe kuvuta dansi hizi, suruali fupi na mambo ambayo watu wanafanya siku hizi, huku kusakata rumba na watusi, na mambo haya yote, kuyapitisha katika Neno la Mungu.

Huwezi kamwe kuvuta hii mitindo mamboleo ya ustaarabu kupitia Biblia. Inaipinga. Waona? Nawe unajaribu kuridhisha hiyo shauku, lakini, waona, ita. . .Hii Biblia itaridhisha tu ladha ya mwanamume au mwanamke mwenye haki. Huyu Roho Mtakatifu, ambaye wangemcheka, na kusema, "Umerukwa na akili." Bali Huyo huridhisha hiyo hamu, jambo hilo ambalo ulimwengu haujui cho chote kulihusu. Wao wamejipotosha wenyewe, kutoka kwa ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu na Neno la Mungu, (hadi wapi?) hadi akaingia katika mashimo ya uchafu, mashimo ya uchafu wa kanisa, wa mafundisho ya sharti na kanuni za imani, na—na tofauti za kidhehebu, na kadhalika.

Wasema "Wewe ni Mkristo?"

114 "Mimi Mmethodisti. Mimi Mbatisti. Mimi Mpresbeteria." Hilo halimaniishi kitu kwa Mungu, hata kidogo. Huwezi kuvuta mambo hayo kupotia hapa Bibliani mwa Mungu. Nawe unajaribu kuridhisha hiyo shauku takatifu ambayo Mungu alikupa, umwonee shauku. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

115 Sasa, mnajua ya kwamba Daudi hapa alisema, "kwa ajili ya Mungu aliye hai." Basi, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Ndipo hakuwezi kuweko uradhi wo wote hata Neno hilo, ambalo ni Mungu, linakuwa hai ndani yako, basi utaona Mungu Mwenyewe akitimiza ahadi alizofanya katika Biblia.

116 Sasa tuna wafasiri mbali mbali wa Biblia. Kanisa moja huifasiri *hivi*, lingine hulifasiri *hivyo*, na lingine *hivi*. Mengine hayachukui ila sehemu dogo tu Yake; wengine huchukua *hapa* na *pale,* sehemu Yake. Bali Mungu hujifasiria Mwenyewe. Anapofanya ahadi na kuitimiza, hiyo ndiyo tafsiri yake.

117 Kama nilikuahidini ningekuwa hapa usiku wa leo, na ndimi huyu, hiyo ni kutimiza ahadi yangu. Kama nikisema nitakutana nanyi asubuhi, nami niwepo, hiyo ni ahadi yangu. Hapana haja ya kutoa udhuru nyingine, inanipasa kuwa pale.

118 Na Mungu anapofanya ahadi, kisha anakuja na kutimiza ahadi hiyo, hiyo ndiyo tafsiri ya hiyo ahadi. Nami ningemhimiza mtu ye yote kusadiki Neno la Mungu, na aone kama kila Neno katika hiyo Biblia si Kweli. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo shauku iliyomo mle.

119 Unasema, "Ningaliishi katika siku za Yesu, ningalitenda *hivi na vile*."

120 Naam, unaishi katika siku Zake. Tunafanyaje juu yake? Tunafanyaje? Unasema "Vema?" Ulivyofanya labda ndivyo Mafarisayo walivyofanya. Wao walikuwa wafuasi wa kanisa, na kumkana Yesu Kristo.

121 Kila mara tunasema siku hizi, watu hujaribu kusema, "Tutalinganisha. Inatupasa kulinganisha ukurasa wa Biblia kwa ukurasa wa Biblia, Andiko kwa Andiko." Hiyo siyo Kweli. La, siyo Kweli. "Hili neno la Kiyunani linamaanisha *hivi*, na *hili* linamaanisha *vile*." Wayunani wenyewe, kule nyuma katika Baraza la Nikea, na hao waandishi kule nyuma, walikuwa na taratibu mbali mbali. Mmoja aliamini hivi, *huyu* mwanachuoni wa Kiyunani alimaanisha *hivi*, na yule mwingine alisema *hili* nalo lilimaanisha *vile*. Nao wakabishania Hilo. Hatuhitaji fasiri ya wanavyuoni wa Kiyunani ama maneno ya Kiyunani.

122 "Kumjua Yeye ni Uzima," Mtu, Kristo Mwenyewe! Si kulinganisha. Ni ufunuo ambao Mungu alijenga Kanisa Lako juu yake. Na kama hatujengi juu ya Kanisa lilo hilo... Biblia ilisema, "Habili, kwa imani!" Na imani ni ufunuo wa Kiungu. Mnaona, imani ni ufunuo wa Kiungu. Sawa. Jambo Hili lote limejengwa juu ya ufunuo basi, na isipokuwa hili limefunuliwa kwako! Yesu alisema, "Nakushukuru, Baba, ya kwamba mambo haya umewaficha wenye hekima wa ulimwengu huu, ukawafunulia watoto wachanga watakaojifunza." Unaona, sasa, jambo hili lote limejengwa pale, huna budi kumjua huyo Mtu!

123 Na hauwezi kuridhisha hiyo kwa kujiunga na kanisa. Huna budi kumpata huyo Mtu, Mungu Mwenyewe, ambaye ni Neno na—na tafsiri Yake leo, ahadi aliyoifanya leo. Watu aliokuwa atawapata siku hizi, "Kanisa lisilo na ila wala kunyanzi," haimaanishi dhehebu fulani; maana yake ni watu, watu binafsi wasio na doa wala kunyanzi. "Kutakuweko wawili kitandani, nitamtwaa mmoja nimwache mmoja, wawili watakuwako kondeni, nitamtwaa mmoja na kuwacha mmoja." Bali wakati Mungu, hiyo shauku takatifu kuwa kama Yeye, kisha unaoana ya kwamba Neno Lake liko ndani yako, likijithibitisha lenyewe, ya kwamba wewe u mtumishi wa Mungu. Lo lote asemalo Mungu, unaandamana nalo basi unapitia njia ifaayo kuridhisha hiyo shauku takatifu iliyo ndani yako.

124 Lo, bila shaka, watu watakuchekelea, wakisema "Umerukwa na akili. Una wazimu." Bali kumbuka wanachonywea, unaona. Angalia waliko. Je, ungeliwazia chemichemi kubwa ikibubujisha maji mazuri, na mtu mmoja akiwa kule chini kwenye moja ya mashimo yale kule, yenye viluwiluwi wafu, na kanuni za imani na kila kitu ndani yake, akinywea kule, akiinua macho yake na kukufanyia mzaha? Lo! Naam, yeye hajui, hajui ji—jinsi kijito unamoishi kinavyotuliza kiu. Hiyo ni kweli hasa.

125 Tuna Mungu aliye hai. Si aliyekufa miaka elfu moja mia tisa iliyopita na akakaa kaburini, bali aliyefufuka tena. Waebrania 13:8, inasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Roho Mtakatifu yule yule aliyeshuka katika Siku ya Pentekoste ni Roho Mtakatifu yule yule aliye hapa sasa. Yeye ndiye Sehemu

iridhishayo, kwa sababu Yeye ndiye Neno. Hiyo ni kweli. Roho Mtakatifu ndiye aliyeliandika Neno, Yeye hufasiri Neno. Biblia ilisema, katika II Petro, ya kwamba Roho Mtakatifu ndiye aliyeiandika Biblia, "Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliiandika Biblia."

126 Sasa, hauwezi kufanya hivyo, hauwezi kuridhisha hiyo shauku takatifu na cho chote kile ila Mungu Mwenyewe akiishi ndani yako, katika Utu wa Roho Mtakatifu. Elimu, utamaduni, kujiunga na makanisa, kukariri kanuni za imani, kuwa mfuasi wa ushirika fulani; mambo haya yote ni mazuri sana, bali hayatakomesha kamwe hiyo shauku. . . hiyo—hiyo shauku takatifu, namaanisha, haitatuliza hiyo shauku takatifu.

127 Nilikuwa nikimsikiza Billy Graham, yule mwinjilisti mashuhuri, usiku uliopita. Nawaambieni, namwombea zaidi sasa kuliko nilivyowahi kufanya, nilipomwona akiwakemea kweli kweli, jinsi walivyofanya. Yeye alisema, "Hilo kundi la makasisi likija barabarani, kala zao zimegeuzwa nyuma!" Wakienda kule ambako haikuwapasa kwenda, wakiingilia mambo yasiyowapasa. Bali walikuwa wakienda barabarani, [Ndugu Branham apiga makofi—Mh.] wakipiga makofi na kufanya vishindo kwa miguu yao. Vema, walionekana kama wasio watakatifu wanaofingirika. Sasa, unaona, bali wana kitu ambacho wa—wanachokiamini. Wana kitu fulani, kinachoamsha nafsi. Wana kitu fulani kinachowafanya washtuke. Mwanamke fulani alienda na kuingiza kichwa chake katika kitu fulani chini kule, nao wakadhani yeye alikuwa mfia dini, naye hakuwa na shughuli mle. Sasa tunaona ya kwamba watu hawa [Ndugu Branham anapiga makofi] walikuwa na kitu ambacho wangepigia makofi. Walikuwa na furaha. Walikuwa wakifanya jambo fulani.

128 Vema, ikiwa unaweza kufanya hivyo kwa ajili ya—ya kanuni unayofikiria ni kweli hapa; kisha usimame kanisani na watu fulani wapige makofi na kufanya vishindo kwa miguu yao, mashemasi wangewatoa nje. Mnaona, wamewaelekeza watu wao kwenye shimo la uchafu wa kanuni za imani na madhehebu, badala la kuwalisha kwa Neno takatifu la Mungu, linalotolewa kwa Nguvu za kufufuka Kwake Yesu Kristo.

129 Mnaona, wao hujaribu kufanya hivyo, wao hutuliza kiu chao kwa kusema, "Mimi ni Daktari *Fulani,*" ama nimetoka seminari fulani ama chuo fulani. Bali hayo hayamaanishi cho chote, hata kidogo. Lakini, mwaona, wao, wao wanajaribu kujiridhisha wenyewe, wakisema, "Naam, Mungu atanitambua kwa maana mimi ni mchungaji Wake. Mungu atanitambua kwa sababu mimi ni Baba mtakatifu *fulani,* ama Askofu *Fulani,*" ama—ama kitu kama hicho. Wao wanajaribu kuridhisha kiu chao hapo, wala huwezi kufanya hivyo. "Nina Ph.D., LL.D., Nilipata Shahada yangu ya Kwanza. Nina *hili.*" Hiyo ni sawa. Bali, kwangu mimi,

hiyo inamaanisha uko umbali huo kutoka kwa Mungu. Hiyo ni kweli. Umbali huo mbali na Mungu, wakati wote!

130 Unajua Mungu tu kwa kuwa na kituko Naye. Hauwezi kujielimisha katika hili. Inazaliwa ndani yako! Ni kitu ambacho Mungu anakupa. Elimu haina uhusiano Nacho. Mmoja wa watu mashuhuri sana katika Biblia hata hangaliandika jina lake, Mtakatifu Petro. Hiyo ni kweli kabisa, yeye pamoja na Yohana, Biblia ilisema, "Wote wawili walikuwa watu wasio na elimu, wasio na maarifa." Bali ilimpendeza Yesu kumpa funguo za Ufalme, kwa sababu alikuwa akimwonea shauku Mungu. Amina. Akimwonea shauku Mungu, ushirika. Naam, bwana. Lo, jamani!

131 Nawaza juu ya Isaya, yule mwanamume kijana, lo, kijana mzuri, alikuwa kule hekaluni, siku moja.

132 Yule mfalme mkuu, naye akamwelekezea uso wake na kufikiri yeye alikuwa mojawapo wa watu mashuhuri sana. Naam, alikuwa mtu mkuu. Alikuwa amekuzwa, wazazi wazuri, mama na baba. Bali alipotoka nje, siasa zake zilikuwa safi, naye alitengeneza mambo yake na Mungu. Isaya alimwangalia na akawaza yeye alikuwa mtu mkuu, akamweka kama kielelezo. Bali usidhubutu (kamwe) kumweka mtu, ila Mwanadamu Kristo Yesu, kama kielelezo chako. Watu wote watashindwa. Baada ya kitambo kidogo, akafikia mahali fulani; yeye alikuwa—alikuwa mfalme, bali akajaribu kuchukua mahali pa kuhani na akaingia hekaluni, naye akapigwa kwa ukoma.

133 Isaya alifadhaika sana, basi akashuka akaenda hekaluni na akaanza ku—kuomba, alifikiri angeshuka aende kule na kuomba kwa muda mdogo. Na sasa, tazama, mtu huyo alikuwa nabii; bali kule hekaluni kulikuwako na kijana mwanamume, alikuwa akimlilia Mungu, siku moja, na ono likamtokea. Na aliyofanya hivyo, akaona Malaika, Makerubi, na nyuso Zao zimefunikwa na—na mabawa Yao, na miguu Yao imefunikwa, huku wakiruka kwa mabawa mawili. Walikuwa wakiruka huku na huko, juu chini kote hekaluni, wakilia "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi."

134 Naye Isaya, ile shauku kuu aliyokuwa nayo, hu—huenda alikuwa ameelimishwa. La—labda alikuwa na elimu nzuri. Alikuwa na mawazo ya ajabu ya jinsi Mungu apaswavyo kuwa. A—alikuwa amewasikia makasisi. Aliisha kuwa hekaluni. A—aliisha kuzwa kuwa mwa—mwamini, lakini, unaona, yeye hakuwa ameiona uso kwa uso hapo mbeleni. Waona? A—alikuwa na hamu ya kutenda yafaayo. Yeye alitaka kuwa sawa, bali alikuwa tu na upande wake wa elimu. Alikuwa na upande wa Hiyo wa kitheologia.

135 Bali alipofika pale hekaluni siku hiyo, na kuwaona hawa Makerubi wakipigapiga mabawa mbele na nyuma, naye akijua kwamba hawa Malaika watumika usoni mwa Mungu; na hao

Malaika hata hawakujua dhambi ni nini, na, kusimama katika Uwepo wa Mungu, iliwapasa kufunika nyuso Zao takatifu, kusimama katika Uwepo wa Mungu. Ndipo huyo nabii akalia, "Ole wangu! kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu. Theologia yangu yote, theologia na mambo niliyosoma, mawazo yangu yote ya ajabu niliyokuwa nayo juu ya Mungu, nimekabiliana nalo uso kwa uso sasa." Yeye akasema, "Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami nakaa kati ya watu wenye midomo michafu." Mafundisho yao yote ya torati, na mambo waliyotenda, havikufikia mahali hapo ambapo alikuja katika Uwepo wa Mungu, na kumwona Mungu kwa macho yake mwenyewe; na pindo la vazi Lake, alipokuwa ameketi Juu sana, kule Mbinguni. Na ndiye huyo, uso kwa uso na kweli. Naye akalia, "Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wachafu."

136 Kisha huyo Kerubi akatwaa makoleo, na kaa la Moto toka madhabahuni, na kuigusa hiyo midomo michafu. Na ikamgeuza toka kuwa mtu mwoga, ama kuwa mtu mwenye elimu, mwalimu, hata akawa nabii ambaye Neno la Mungu lingenena kupitia kwake. Bila shaka, alipokuwa katika Uwepo wa Mungu, ilikuwa Jambo tofauti. Ile shauku aliyokuwa nayo, ilikuwa imeshafikia mahali hapo basi, hata akajazwa Nayo.

137 Na hebu nikwambie, rafiki, sijali utajiunga na makanisa mangapi, utajiandikisha majina mangapi, njia utakayopitia, na kama umenyunyiziwa maji, umebatizwa, ama vyo vyote ulivyo; hata utakapokutana na Mtu huyo, Yesu Kristo! Hicho, hicho ndicho kitu pekee kitakachoridhisha kabisa.

138 Mwamsho hautafaa; huenda ukaruka juu-chini na kupaza sauti upendavyo, ama huenda ukakimbia huku na huko sakafuni, na huenda ukanena kwa lugha utakavyo. Na mambo hayo ni matakatifu na mema. Sisemi—sisemi neno kinyume cha hayo. Bali hata utakapokutana na Mtu huyo, hiyo Sehemu iridhishayo, Kitu hicho ambacho kitatwaa kila uzi mwilini mwako; si kwa mwamsho, bali kwa uradhi!

139 Nilizoea kuona alama iliyosema "Ukiona kiu, sema Parfay." Kilikuwa kinywaji kidogo, nilipokuwa mvulana, kilichoitwa Parfay. Nakumbuka nilipokuwa naja barabarani, lo, toka kuvua samaki, nilikuwa huko kwenye kidimbwi, maji ya kale machafu. Nami nusura nife kwa kiu, nami nikaona hiyo alama iliyosema, "Ukiwa na kiu, sema tu Parfay." Nami nikaanza kusema, "Parfay, Parfay." Nikazidi kuwa na kiu. Na—nami . . . Unaona, ni—ni—niliona kiu sana hata singalitema mate, baada ya kitambo kidogo, ni—nilikuwa na kiu sana.

140 Vema, waona, hiyo haifai kitu. Hamna kitu kitakachoiridhisha. Sijali, unaweza kunywa kokakola, na unywe cho chote utakacho, ambazo zimetiwa utamu kwa soda, na kadhalika, hamna kitu kitakachoridhisha kiu kama maji mazuri

na baridi ya mtoni. Hayo yatatuliza hicho kiu. Vitu hivi vingine vyote ni mabadilisho.

141 Na mbona tungetaka kuchukua badilisho, na kuna ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu ambao huridhisha kila hali na hamu nafsini mwa binadamu? Kisha unakabiliana na mauti, kama yule Mtume mkuu Paulo alivyosema, "U wapi, ewe mauti, uchungu wako? Na, kaburi, kuwapi kushinda kwako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo!" Hicho ndicho kituko, ndugu, kinachoridhisha hiyo tulizo takatifu ambayo . . . ama hiyo shauku takatifu iliyo ndani yako. Huiridhisha. Haikupasi kufanya kingine cho chote juu yake. Naam, inatakasa midomo.

142 Na pale pia, kuna watu tu wanaoishi kwa mwamsho, juu ya . . . Watu wengine husema, "Vema, tuna mambo mengi kama hayo katika dhehebu letu la Kipentekoste." Nao wataingia, ambayo ni sawa, watapiga makofi [Ndugu Branham anapiga makofi—Mh.] na kucheza muziki. Muziki unakwisha, "sh, whiuu," ndoo ya maji ilimwagiliwa juu ya kila kitu, waona. Sasa tu—tunafanya hivyo, tu—tumezoea kufanya hivyo. Tuna, tu—tu . . . Imekuwa moja ya desturi zetu.

143 Hebu niwaambieni kitu. Mnapomwabudu Mungu, katika Roho na Kweli, inapokuwa *desturi* yenu kufanya hivyo, maana mnafikiri *inawapasa* kufanya hivyo; kwa sababu unafikiri, kama hamtapiga makelele, ama kuruka juu-chini, ama kucheza kwa muziki, jirani yenu atafikiri mmeanguka; mnakunywa kutoka kwa mto uliochafuka. Kweli!

144 Mpaka Yeye atakapoujaza kila sehemu, hata Roho Mtakatifu Mwenyewe atakapokuwa anabubujika ndani yako; sijali kama muziki unacheza, au wanacheza *Karibu na Wewe, Mungu Wangu*, ama cho chote kile, Roho Mtakatifu yuangali anapiga kengele za utukufu moyoni mwako, Hiyo inaridhisha. Hiyo ndiyo Sehemu ya Mungu inayoridhisha. Cho chote chini ya Hiyo, umekwisha.

145 Huenda ukanena kwa lugha kama wanadamu na Malaika, huenda ukatoa mali zako kuwalisha maskini, huenda ukatoa unabii, na huenda ukawa na maarifa, kujua siri zote na mambo haya yote, na bado utakuwa si kitu wewe (I Wakorintho 13) hata Kitu hicho kinachoridhisha ambacho ndicho tu kinachoweza kutuliza hicho kiu.

146 "Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu aliye hai, kama ayala auoneavyo shauku mto wa maji. Nisipompata, nitaangamia." Unapoanza kumwonea Mungu njaa hivyo, jambo fulani litatendeka. Roho Mtakatifu atakuongoza hata kwenye zile chemchemi kuu za Mungu. Naam, bwana.

147 Naam, hilo ni jambo nzuri, kuabudu katika Roho. Hiyo ni kweli. Bali wakati mwingine una Roho bila Kweli. Yohana Mt. 4, ilisema, "Tunamwabudu Mungu, kwa Roho na Kweli." Naye Yesu ndiye Kweli. Hiyo ni kweli hasa. Naye ndiye Neno.

148 Mito ya Mungu iliyotumwa kukuridhisha, katika mwili, Shetani alichafua kila mmoja wayo. Ametia dawa ya sumu katika kila mmoja angaliweza kuingia kwake. Hiyo ni kweli. Aliutwaa ule mto mkuu, wa kanisa.

149 Hiyo, hiyo ilikuwa ndiyo njia ya Mungu. Yesu alisema, “Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda.”

150 Sasa kuna ubishi mbalimbali juu ya hayo. Warumi, Wakatoliki husema, “Yeye alilijenga juu ya Petro.” Mwaona, na kama hiyo ni kweli, Petro alianguka katika aibu. Kwa hivyo, haikuwa hivyo. “Hilo,” bila shaka halikujengwa juu ya Petro, *Petra,* jiwe ndogo. Kisha Waprotestanti husema, “ya kwamba Yeye alilijenga juu Yake, Yesu Kristo.” Sikusudii kuwa tofauti, bali sikubaliani nao. Yeye hakulijenga kamwe juu ya ye yote wao.

151 Yeye alilijenga juu ya ufunuo wa Yeye ni Nani. Yeye alisema, “Heri wewe Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili.” Si kwa maarifa! Haukujifunza haya kwa vitabu. Haukujifunza kwa kujiunga na kanisa. Haukujifunza haya madukani. Hukujifunza! Bali Roho Mtakatifu Mwenyewe ameuleta Utu wa Yesu Kristo kwako, basi, “Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda.” Hicho kiu kitakatifu kimeridhishwa katika Utu wa Yesu Kristo. Ndivyo hivyo. Hicho ndicho kitu tunachotaka kutafuta, kuridhisha hicho kiu Kwake. Sawa, tunaona ya kwamba hatuna budi.

152 Maarifa? Lo, jamani! Maarifa ni jambo kuu, tunayojaza, na siku hizi tunayo chungu nzima. Lakini unaona, maarifa . . . kama nilivyokuwa nikisema hivi majuzi, nikinena juu ya maarifa. Kulikuwako na mtu aliyesimama nje, alikuwa anazungumza na rafiki yangu aliyesimama huko, kasema, “Kama mtu haamini katika elimu, mbona anasoma Biblia?” Wao . . .

153 Nikawaza, “Vema, kama hawakufahamu aliyosema Bwana Yesu, watafahamuje yale mjinga kama mimi ninayosema?” Hata hawangalimfahamu Yeye, ingawa alikuwa dhahiri sana.

154 Yeye alisema kule siku moja, “Msipoula mwili, Damu, kuinywa na kuula mwili wa Mwana wa Adamu, hamna Uzima ndani yenu.” Yeye hakuieleza. Akaendelea mbele. Hiyo ni kweli. Waona?

155 “Vema,” wao walisema, “Mtu huyu ni mla watu. Tunamtaka Yeye . . . kula mwili Wake, kuinywa Damu Yake. Yeye ni kizuu kifyonza damu. Waona, Yeye anatutaka tuwe kizuu kifyonza damu.” Waona hao wenye elimu!

156 Bali Yeye alisema, “Kondoo zangu huisikia Sauti Yangu.” Waona ingewajia walio Wateule, waliteuliwa na Mungu kwa kujulikana tangu asili. “Na wale ambao Baba . . . Hakuna mtu

awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba. Na wote alionipa Baba watakuja, watalifahamu."

157 Hao wanafunzi hawangalililifahamu, bali walilliamini. Waona? Hiyo ni kweli. Kama ukiliamini! Siwezi kufahamu mambo mengi. Naliamini, kwa vyo vyote, waona, kwa sababu Mungu alisema ndivyo ilivyo.

158 Maarifa. Mwajua, injili ya Shetani ni maarifa. Je, mlijua hivyo? Aliihubiri katika bustani ya Edeni, kwa Hawa, naye akadanganyika kwa injili yake ya maarifa. Sasa, naye amechafua jamii yote ya binadamu, kwake. Hiyo ni kweli hasa. Wao wamechukua mipango ya elimu, wakaiweka kanisani. Hiyo ni sawa *huko* nje, bali si katika Neno la Mungu. La, bwana. Haumjui Mungu kwa elimu. Haumjui Mungu kwa—kwa—kwa kisomo, kujifunza hesabu na kutamka maneno makubwa.

159 Paulo, alikuwa mtu mwerevu. Bali alipomjia Kristo, na kumpokea Roho Mtakatifu, alienda kwa Wakorintho, akasema, "Sikuja kwenu kamwe kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu," ingawa yeye angalifanya hivyo. Kasema, "Nalikuja kwenu kwa nguvu na kwa dalili za Roho Mtakatifu, ili imani yenu iwe katika Mungu, si katika hekima ya mtu fulani."

160 Sasa mara kwa mara tunatayarisha mipango ya kanisa, wao pia humwita mchungaji wa—wao. Kanisa linaenda kumpigia kura mchungaji, wao wanasema, "Vema, mchungaji huyu, sasa, yeye amepata shahada mbili chuoni. Alisoma saikolojia miaka minne. Alisoma *hili, lile, linginelo*." Nao watampigia kura mtu kama huyo (kwa nini?) badala ya mchungaji anayeamini Neno la Mungu lina upako nalo ni Mungu, naye atalihubiri Neno bila kujali vile watu waonavyo.

161 Mungu alimwambia Ezekieli, kasema, "Hubiri waamini wasiamini. Lihubiri, kwa vyo vyote." Waona? Sawa. Waamini wasiamini, si hoja. Wao hawakumkubali Yesu. Aliendelea tu, akilihubiri vivyo hivyo. Waona?

162 Badala ya mchungaji halisi ambaye atalihubiri Neno na kumwamini Mungu, wao—wao—wao hujaribu kuingiza a—akili, mtu aliye na elimu bora sana; mtu anayeweza kusimama mimbarani na hatachukua ila dakika kumi na tano, kusudi wapate kurudi nyumbani upesi sana, na kuenda (baadhi yao) kufanya jambo lingine, naye Mlaghai anaweza kutwaa bunduki yake ya kale na kuondoka, nao wanaweza kwenda kwenye karamu za dansi na kadhalika. Na ni, lo, ni—ni—si kitu ila unajisi wa mchanganyiko wa elimu. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyo hasa. Hiyo ni kweli. Lakini ni nini? Huridhisha radha yao, waona huridhisha radha ya washirika wa kanisa la kilimwengu.

Hairidhishi ladha ya mtu mtakatifu. Yeye atachukua Neno kila wakati!

163 Bali wao husema, “Lo, hao watu wamerukwa na akili kidogo. Waona, hawafanyi hivyo, hawalifahamu. Wao, wao wanajaribu kuishi katika siku zilizopita.”

164 Si ajabu hiyo! Mimi huja humu Magharibi, nami naona wao wanajaribu kuishi katika siku zilizopita, wao kila mara wanataka kuishi katika siku za mtindo wa kale, za wachunga ng’ombe. Hebu nenda kule Kentucky, siku za kale za kimwitu, wanataka kutenda kuziigiza, kufanya mipango yake. Bali ifikiapo ile Dini ya mtindo wa kale, hawataki chochote chake.

165 Siku za mtindo wa kale? Nilikuja huku mnamo wakati wa maonyesho ya ujuzi wa wachunga ng’ombe, nikaona walikuwa na mwanamke mkubwa kule, mwenye rangi kijani kibichi chini ya macho yake, na nywele fupi zilizokatwa, sigara mdomoni mwake. Naam, kama wangaliona hayo siku za kale, wangalidhani alikuwa ameoza mahali fulani. Wao, wao wa—wa—wangalimfunga jela. Vipi kama mama yako angalitoka nje, amevalia jinsi wewe na bintiyo mnavyovalia siku hizi, ingekuwaje? Wangalimpeleka kwenye hospitali ya wenda wazimu. Bila shaka alitoka nje bila rinda. Vema, sasa kumbuka, ni jambo lile lile siku hizi.

166 Wanadamu wameoza miilini mwao. Kama wanakuwa na umri wa makamu, kati ya miaka ishirini na ishirini na mitano, chembechembe za bongo wao zinaoza pia. Hawana . . . Watu wamefikia mahali ambapo hawana ufahamu wa kutosha. Hawajui maana ya adabu. Hawajui tofauti ya mema na mabaya. Na, lo, ingawaje, mipango yao ya elimu, wao . . .

167 Je, mlijua, elimu, naweza kuwathibitishia, ni ya Shetani? Si kusoma na kuandika; bali, namaanisha, kuingiza elimu yao kanisani mwenu.

168 Je, ukomunist hutegemea nini? Sayansi, elimu, huyo ndiye mungu wao. Shetani, waona, hayo ndiyo aliyomjulisha Hawa. Hayo ndiyo wangali wanayashikilia.

169 Sasa yameingia makanisani mwetu, yameingia kwa Wabatisti, Wamethodisti, na Wapresbeteria, Wapentekoste, na wote hao. Elimu fulani, akili, kitu *fulani* kikuu na mambo kama hayo, ambayo humtupilia mbali zaidi na Mungu. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Sasa, tunaona, ya kwamba (wao) inaridhisha tamaa zao. Wakati—wakati ka—kanisa linapochagua kwa kura kitu kama hicho, inaonyesha ni nini kilicho katika nia ya hilo kanisa, kilicho tamaa yao, kile wanachoonea kiu. Wao wanataka kusema, “Mchungaji wetu ana maarifa mengi. Yeye hajali kama tukiogelea waume kwa wake, naye huenda pamoja nasi.”

170 Msichana mdogo alimwambia Sara wangu, hivi majuzi. Mchungaji wake alikuwa amezuru Afrika; na aliporudi; huyu msichana akavua nguo zake, usiku huo, akiwa na suruali ndefu iliyombana, na kumchezea watusi, kumtumbuiza kwa sababu alikuwa amezuru Afrika. Watusi ni kabila fulani kule, mwajua.

Jamani, singetaka kuona mmoja wa wasichana wangu, katika kusanyiko langu, akijaribu kufanya jambo kama hilo, watusi?

171 Unaona, hiyo inaithibitisha! Mchungaji ambaye angeketi na kumwangalia mmoja wa kusanyiko lake, maskini msichana (mwenye umri wa miaka kumi na sita) kule uchi hivyo, na kumwachilia aendelee hivyo, hiyo inaonyesha ya kwamba huyo ametoka kwenye shimo la uchafu, mwenyewe, mtu wa Mungu akifanya jambo kama hilo. Bila shaka.

172 Hilo laonekana halipendezi, bali najua ninahubiri kote nchini, pia. Bali mnajua hili pia, ndugu, dada, hebu niwaambieni, hiyo ni Kweli.

173 Nderi anataka vitu vilivyokufa. Hiyo ni kweli. Na hicho kimekufa! Hiyo ni kweli hasa. Inaonyesha dhahiri, inaonyesha tu dhahiri hapa kichwa chao na mnara wao wa kusimama ni nini, kile unachowapa, waona, kile kilicho nafsini mwao. Nafsi zao zinatamani mambo kama hayo.

174 Nafsi zao hutamani kanisa la hali ya juu na ya kiakili, ambamo watu huvalia nadhifu sana, naye mchungaji huchukua dakika kumi na tano, ama ishirini. Nawe ukipitisha hizo, wanamtupa kwenye halmashauri ya mashemasi. Naye hapaswi kusoma neno juu ya dhambi. Asiseme cho chote kuhusu kuvalia suruali fupi, naye hatasema lo lote kuhusu watu kufanya *hivi, vile,* au *vingine*. Haimpasi kutaja hayo kamwe. Wakifanya hivyo, halmashauri itamfukuza. Unaona jinsi mambo yalivyo? Hilo ndilo chujio lao la mtu mwenye busara.

175 Biblia ilisema, katika I Yohana 2:15, "Ukipenda utaratibu wa ulimwengu huu, ama mambo ya ulimwengu huu, ni kwa sababu upendo wa Mungu hata haumo ndani yako."

176 Sasa vipi kuhusu mambo haya yote yasiyofaa waliyo nayo siku hizi, katika jina la kanisa; wakifanya mazoezi ya dansi mraba kanisani, kamari, karata, karamu, rumba za vijana, dansi, upuzi huu wote! Mtazameni huyu Elvis Presley, ibilisi anayesimama amevalia viatu! Pat Boone, Rickey Nelson, kizuizi kikubwa sana taifa hili lilichopata kuwa nacho! Hiyo ni kweli. Wao husema, "Lo, wao ni wa kidini sana, waliimba nyimbo za Kikristo." Si halali, kanisa halipaswi kukubalia kitu kama hicho! Baadhi ya hawa watu huja humu, na—na usiku wa leo wamo katika ho—hoteli hapa, wakicheza dansi na kupiga muziki na kila kitu, na usiku unaofuata wanakuja madhabahuni na kulia machozi, na usiku unaofuata wanacheza muziki jukwaani. Lo, alhamdu lillahi! Uchafu unaweza, uchafu unaweza kwenda umbali gani, kwa kila hali? Naam, bwana. Athibitishe mwenyewe kwanza kuwa ni mtu wa Mungu, si upuzi huu wote eti kwa sababu tu anacheza gitaa ya kale ama cho chote kile.

177 Kwa tamaa yako, unaweza kujua ni nani anaye kalia kiti moyoni mwako. Kwa yale unayopenda, hayo ndiyo huonyesha.

Wewe, wewe wasema, “Vema, nafikiri mambo hayo ni sawa, Ndugu Branham.” Vema, kumbuka tu sasa, moyoni mwako, unajua kilichoko. Ndiyo, bwana. Kwa kile kinachoilisha nafsi yako, kile nafsi yako inachoonea kiu, na waweza kuona inaridhisha hicho; kama si Neno hili, basi kuna kasoro, kwa sababu Roho Mtakatifu huishi kwa Neno tu. Waona?

178 Nataka muone hatari nyingine, kabla tu hatujafunga, kama huna—kama huna hatia ya mambo hayo yote nimetaja, na, hiyo ni, hatari ya kutojali kiu. Unaona? Unasema, “Nina kiu kitakatifu. Bali si—sina hatia, Ndugu Branham, ya kwenda tu na kujiunga na kanisa, na mambo kama haya.” Bali, waona, kutojali kiu! Kama usipojali kuridhisha kiu cha maji au chakula, utakufa. Na kama ukikosa kujali hicho kiu ndani yako, cha Mungu, utakufa kiroho.

179 Mnaweza kuombea ufufuo, mngojee kanisa lenu liwe na ufufuo. Vema, huo—huo si ufufuo kwenu. Ufufuo unapaswa kuanza ndani yako, unapoanza kumwonea kiu Mungu. Huenda kusiwe na mshiriki mwingine, wa kanisa, anayehitaji huo ufufuo. Ukianza ndani yako, utaanza mahali pale pengine. Unaona? Lakini, unaona, unakosa kujali hicho kiu.

180 Usipojali kumkama ng’ombe, wakati ng’ombe ana . . . kiwele kimejaa maziwa; na ukimwacha huyo ng’ombe akae hivyo, atakauka. Hiyo ni kweli hasa. Usipojali kunywa maji, useme, “Sitayanywa tena,” utakufa. Usipojali kula chakula, utakufa.

181 Kwa hivyo usipojali kumpa Roho Mtakatifu Neno la Mungu, utakufa.

182 Enyi Wakristo, enyi Wabatisti, Wamethodisti, Wapresbeteria, Wapentekoste, Assemblies of God, Waumoja, Wauwili, Wautatu, cho chote ulicho, unaona; sijali, hilo halidhuru kwangu, sidhani linadhuru kwa Mungu. Unaona, wewe ni mtu binafsi, wewe ni mtu mmoja. Hautaenda Mbinguni kama kanisa, dhe—dhe—dhehebu. Utaenda Mbinguni kama mtu mmoja pekee, wewe na Mungu. Hivyo tu. Sijali wewe ni wa kanisa gani.

183 Na kama hutajali kusoma Biblia na kuamini Biblia, na Roho Mtakatifu kulishwa Hiyo, utakufa. Yesu alisema katika Yohana Mt . . . 4:3, Andiko nimelipata . . . Yesu alisema kwamba, “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno,” si sehemu Yake tu.

184 Tunachukua kidogo *hapa*. Naita hayo kuomba lifti kwa Biblia. Wao husema, “Vema, naamini *Hili,* bali hebu tuende *hapa* waona.” Unaona?

185 Huna budi kulichukua, Neno kwa Neno. Yesu alisema, “Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Unajua hivyo? [kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

186 Na, wajua, tumefanya—tumeifanya siku tunamoishi, tu—tumeifanya siku hii . . . u—u—upotovu wa kidini.

187 Binti yangu aliniita, si muda mrefu uliopita, akaniambia, “Baba,” upande mwingine wa nyumba, kasema, “njoo hapa, tutakuwa na kipindi cha kidini.” Ilikuwa nyimbo, kuimba nyimbo za dini, na kulikuwa na maskini Mlaghai, akisoma pale. Na kama nimewahi kuona mwenendo wa kukufuru, ulikuwa huo! Hao watu kule, na watu, ilionekana kama kwamba ilikuwa kama maonyesho ya wacheza muziki wa kilabu cha usiku. Ilikusudiwa kuwa kabila fulani la Kihindi, nao walikuwa wakifanya yasiyofaa, na—na kuruka juu na kupigana makonde.

188 Naam, je, ule unyofu wa moyo ulienda wapi, ziko wapi zile nyimbo za mtindo wa kale tulizozoea kuziimba, na kufurahi katika Roho wa Mungu huku machozi yakitiririka mashavuni mwetu. Na sasa tunajaribu kuzuia pumzi hadi hatuna pumzi ya kutosha ndani yetu, hata nyuso zetu zinageuka kuwa samawati, kujaribu kuonyesha ya kwamba sisi ni waimbaji wa aina fulani. Mnaona, tumeiga hayo kutoka Hollywood, na vipindi hivi tunavyoona kwa hizi nyimbo za kiakili na kuzoeza sauti. Na—napenda kusikia uimbaji mzuri, napenda kusikia uimbaji mzuri wa mtindo wa kale wa kipentekoste, unaochangamsha moyo. Bali bila shaka nachukia kusikia huko kulialia kweche kweche wanakokuita kuimba, leo. Hiyo ni kweli. Nafikiri hiyo ndiyo dhihaka kuu sana. Ni upotovu. Hiyo ni kweli.

189 Napenda kumwona mwanamume akiwa mwanamume. Nachukia kumwona mmoja akiwa na nguo za ndani za mkewe kule nje, zilizolegea upande mmoja; na—mkunjo umening’inia hapa mbele, na misuko miwili ya nywele ikining’inia kama miraba, ikining’inia usoni. Huyu si—singalimwita huyo mwanamume. Hajui yeye ni wa taifa gani. Waona? Hiyo ni kweli. Unamwona mwanamke, tazama, mwanamke huyo anajaribu kukata zake, kuzifanya nywele zake kama za mwanamume; mwanamume anajaribu kufanya nywele zake, zining’inie usoni kama za mwanamke. Mwanamume amevalia nguo za ndani za mkewe; naye mkewe anavalia ovaroli zake. Waona ni upotovu, kila mahali.

190 Na ni vivyo hivyo kwa taifa, kwa watu, kwa makanisa, kwa kila kitu. Ee, Mungu! Mwisho wa mambo haya uko wapi? Kule Kuja kwa Bwana Yesu Kristo, huo ndio mwisho wake.

191 Kwa hivyo, usipojali kumlisha Roho Mtakatifu Neno la Mungu! Yesu alisema, “Kila Neno litakuwa kwa Roho Mtakatifu.” Basi sikizeni sasa. Ukijaribu kumlisha kitu kisichofaa, kama ni Roho Mtakatifu halisi aliye ndani yako, atajua tofauti yake. Na, kumbuka, Neno la Mungu ndilo Roho Mtakatifu analolishwa. Halishwi shauku. Halishwi elimu. Halishwi kuhudhuria kanisa. Halishwi theologia. Kuna tofauti kubwa kati ya kitu kilicho na uvuvio na msimamo wa kitheologia.

192 Na hao wanatheologia wote katika siku za Yesu, jamani, walikuwa na neno kwa neno, kurasa kwa kurasa, yote yalipangwa, ilimpasa Masihi kuja *hivi!* Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa. Nao, kila mmoja, akakukosa. Unajua aliyosema Yesu alipokuja, kasema, "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na kazi zake ndizo mfanyazo."

193 Haikufunuliwa kwao Neno halisi lilikuwa nini. Mwaona, walikosa hizo kona ndogo, kama wanavyozikosa leo. "Kama utakuwa mfuasi wa *hili* na mfuasi wa *lile,* utakuwa sawa." Usiamini hivyo. Inakupasa kuwa wa Kristo. Na ikiwa kuna Kitu fulani ndani yako, kinachomwonea njaa Kristo!

194 Kumbuka tu, ulipokuwa viunoni mwa baba yako, ulikuwa pamoja naye wakati huo. Bali baba yako hakukujua wakati huo, nawe haukumjua baba yako. Nawe ilikupasa uje uzaliwe. Mungu alikutengenezea njia kupitia kwa mama yako, tu—tumbo la uzazi kisha ikaja. Ndipo ukawa mwanamume ama mwanamke, cho chote kile, halafu ukamtambua baba yako, naye babako angekuwa na ushirika pamoja nawe.

195 Sasa, kumbuka, kama una Uzima wa Milele, Uhai wako ulikuwa ndani ya Mungu hapo mwanzo. Na, Uhai, Mungu ni Neno. Kisha Neno lilipofanyika mwili katika Yesu Kristo, Mungu akishuka chini kuishi katika mwili Wake Binafsi, akajifanya Mwana wa Mungu. Mungu aliposhuka kukaa katika huo, ulikuwa ndani Yake aliposulubishwa. Nawe ulisulubishwa pamoja Naye, na ukafa pamoja Naye Kalvari. Ulizikwa pamoja Naye, mlimani. Nawe ulifufuka pamoja Naye, katika ile asubuhi ya Pasaka. Na sasa unaketi pamoja Naye katika Ulimwengu wa Roho, ndani Yake, na sasa una ushirika pamoja Naye. Waona?

196 Mungu Mwenyewe akawa mmoja wetu. "Hakuna mtu aliyemwona Baba, wakati wo wote, Mwana pekee wa (Mwana) Baba, huyu ndiye aliyemfunua." Hiyo ni kwamba, Mungu akafanyika mtu, apate kushiriki na mwanadamu. Waona? Nawe ni—wewe ni mwili, Naye ni mwili. Mungu aliyefanyika mwili kwetu, katika Utu wa Mwanawe, Yesu Kristo. Na ndani Yake mlikuwemko Mungu. Yeye alikuwa Mungu, si kitu ila Mungu. Yeye alikuwa Mungu. "Mungu aliyedhihirishwa katika Mwana, Yesu Kristo," ambayo ilimfanya *Imanueli,* kama vile nabii alivyosema angekuwa.

197 Sasa waona, basi, ilikupasa uwepo kabla ulimwengu haujaumbwa, jina lako liliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Basi waweza kula nini? Roho Mtakatifu huishi kwa Neno la Mungu. Na sasa katika Ufunuo 22:19, Biblia ilisema, "Ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka kwa *Hiki,* ama aongeze neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima." Unaona ilivyo na kilindi? Huwezi, Roho Mtakatifu hataishi kwa mambo ya ulimwengu.

198 Kama hua ndege na kunguru. Kunguru ni mnafiki mkuu. Kunguru, kiumbe hicho kinaweza kwenda kule nje na kula ngano siku nzima; na aende kule na kuurukia, mzoga wa kale uliooza, na kuula pia. Anaweza kuketi kondeni na kula pamoja na hua, ngano, na kwenda kule na kula mzoga uliooza.

199 Bali hua anaweza kula ngano siku nzima, bali hawezi kula mzoga uliooza, kwa maana yeye ni hua. Naye hua hana nyongo yo yote. Kuuma mara moja kwa huo mzoga uliooza, kungemuua huyo hua. Unaona, hana nyongo. Na hivyo ndivyo alivyo, hana uchungu.

200 Na hivyo ndivyo alivyo Mkristo halisi na wa kweli. Hawataki mambo ya ulimwengu. Wao hula tu Neno la Mungu, na Hilo tu; lililo safi, Chujio la mtu mwenye hekima. Unaona, wao hupitia kwa Hilo, na Hilo pekee. Mambo ya ulimwengu yaliyokufa, yananukia kwao.

201 Mtazame maskini kunguru huyo wa kale katika zamani za baada ya yale maangamizi ya gharika, akiruka toka kwenye mwili mmoja hata mwingine, akila maskini mizoga ya kale iliyooza, hakurudi safinani. Bali yule hua hangalipata mahali pa kupumzisha miguu yake, waona, alirudi safinani alikokuwa akipata nafaka. Na hivyo ndivyo tufanyavyo, tunaishi kwa Neno la Mungu.

202 Katika Zaburi 42. Hapana budi Daudi aliandika hii Zaburi, Zaburi 42, alipokuwa mtoro, aliposema, "Nafsi yangu inakuonea kiu, kama ayala aoneavyo shauku mto wa maji." Tazama, alilia. Daudi alikuwa mtoro. Aliisha kuwa . . . Alikuwa ametiwa mafuta, alijua atakuwa mfalme. Nabii alikuwa amemtia mafuta kuwa mfalme. Sasa tazama, na ndiye huyo, alikuwa na kundi ndogo la askari, wa Mataifa, na kadhalika, alikuwa juu ya mlima. Ambapo, mji wake mpendwa, kwa ajili ya dhambi zao, walikuwa wamezingirwa kote na Wafilisti. Naye Daudi, katika hiyo siku yenye joto, hapana shaka ndipo alipoandika hii Zaburi, "Kama ayala aioneavyo shauku mto wa maji."

203 Tazameni Daudi katika hali hii. Yeye alitazama chini, akauona mji wake alioupenda. Naye akakumbuka alipokuwa mvulana mdogo, alizoea kuwapeleka kondoo kule karibu na hiki kidimbwi kule. Ilikuwa nchi yenye maji mengi sana, pia yenye chakula, kule. Kweli, *Bethlehemu* maana yake ni "nyumba ya chakula cha Mungu." Kisha Daudi alipokumbuka alipopitia kule na kunywa maji hayo baridi, naye ndiye huyu amelala hapa sasa, mtoro, mbali na watu wake. Hakuwa na mahali pa kwenda, na nafsi yake hapana shaka iliyalilia hayo maji mazuri na baridi.

204 Alikuwa na baadhi ya watumishi hapo ambao, jamani, shauku yake iliyo ndogo sana ilikuwa amri kwao. Nao, watatu wao, walipigana kupitia mlolongo wa Wafilisti; maili kumi na tano, maili saba, ama cho chote kile, mbele na nyuma; wakifanya

njia kwa upanga, hata wakamletea maji ya kunywa. Bali nafsi huonea kiu . . .

205 Mwili wake yeye alikuwa juu kule, huenda ikawa ilimbidi kunywea cho chote angalishika, baadhi ya ngozi za kale za mbuzi na kadhalika, zikiwa na maji moto, kwenye hiyo siku yenye joto. Aliwazia, "Laiti ningaliketi chini na kutuliza kiu hili nilicho nacho! Laiti ningalishuka kwenda kule Bethlehemu na kulala karibu na ile chemchemi, na kuyanywa!"

206 Na walipotelemka na kupata hayo maji; na kuyaleta, shauku ya nafsi yake ilikuwa kuu zaidi, si kwa ya Bethlehemu, bali ya kutoka Yerusalemu; nafsi yake ilikuwa hivyo. Kwa hivyo akayatoa hayo maji sadaka, kasema, "Hata sitayanywa." Akayamwaga juu ya nchi. Mnaona, nafsi yake ilimwonea kiu sana Mungu, kuliko kutuliza kwa . . . kiu cha mwili wake, kwa maji mazuri na baridi. Akayamwaga juu ya nchi.

207 Mnaona, Nyumba ya Mungu, maji yanayopoza nafsi, ya Yerusalemu iliyo juu! Yesu alisema, katika Yohana 6:33, "Mimi Ndimi Chakula cha Uzima. Mimi ndimi Chakula cha Uzima." *Bethlehemu,* "nyumba ya Mungu," kanisa letu, kanisa la duniani la Mungu, kanisa lililoko hapa duniani. Tunapenda kwenda kanisani hapa ulimwenguni, bali iliyo kuu sana ni Yerusalemu, iliyo juu, ambayo ni Mungu. Yerusalemu ya juu, ambayo ni Mungu! Kiu cha nafsi hiyo ndicho kikuu sana, kuwa kule pamoja Naye, kuliko ingalivyokuwa kujiridhisha tu mwenyewe kwa kujiunga na kanisa mahali fulani. Unaona, kujiunga na kanisa hakuridhishi kiu hicho. Daudi alithibitisha hayo hapa, na yale maji yatokayo moja kwa moja kwa nyumba ya Mungu, waona, aliyamwaga juu ya nchi; kupata kibali, kupata kinywaji kizuri baridi kutoka kwa Mungu. Hata juu ya hayo . . . Kilicho kikuu kuliko kiu ulicho nacho, ni kiu hicho cha nafsi iliyo na kiu cha Mungu.

208 Tazameni Yerusalemu, lile Neno. "Yerusalemu imetoka juu," Biblia ilisema, "ambayo ndiyo sisi . . . ni Mama yetu sisi sote." Naye Kristo ni Mama yetu. Tunatambua ya kwamba Mungu ni Mama yetu, kwa maana tumezaliwa Naye. Neno hilo linamaanisha "amani," Yerusalemu, *Shalom.* Ama, *Shalom,* ambayo maana yake "amani," Yeru-shalom, waona, maana yake ni "amani."

209 Kiu kikuu cha nafsi yo yote kinapaswa kuwa maji ya Uzima, kuliko kusema wewe ni mfuasi wa kanisa; kiu cha nafsi hakiwezi kuridhishwa, kiu halisi na cha kweli. Hakiwezi kupotoshwa. Unaweza *kufikiri* uko sawa unapojiunga na kanisa, bali sivyo. Hiyo haitaridhisha kiu halisi na kitakatifu cha Mungu. Haiwezi kamwe. Hai . . . Haiko pale.

210 Sasa Daudi alisema, katika Zaburi 42:7 hapa, "Kilindi chapigia kelele Kilindi kwa sauti ya maporomoko ya maji Yako," kilio cha nafsi.

211 Tazameni, nimetumia hii mara kwa mara kueleza kwa mfano. Kama kuna pezi mgongoni mwa samaki, lilipaswa kuwekwa mle apate kuogelea kwake. Analihitaji. Sasa kama angalisema, "Nitakuwa samaki tofauti. Nitakuwa samaki mwerevu, mwenye elimu. A-haa, ni—nita . . . nitaamini theologia halisi! Naamini si lazima niwe na hilo pezi"? Hangeenda mbali sana majini, angeenda? Na hiyo ni kweli kabisa.

212 Vipi kama mti ulisema "Naam, najua kulipaswa kuwe na dunia kwanza, nipate kukulia mle. Hiyo ni kweli. Ninapaswa kukulia hapa. Bali nitakuwa mti tofauti, nawataka waniweke papa hapa barabarani, kusudi nionekane"? Unaona, hungaliishi mda mrefu sana. Waona? Hiyo ni kweli.

213 "Kilindi kinapopigia kelele Kilindi." Inahitaji zaidi ya kujiunga na kanisa. Ni zaidi ya kusalimiana kwa mikono na mhubiri. Ni zaidi ya kuishi maisha mazuri na mema. Inahitaji kitu fulani kikuridhishe humo ndani, kinachomiminika kutoka kwa Mungu, kuingia nafsini. "Kilindi kikipigia kelele Kilindi, kwa sauti ya maboromoko ya maji Yako, Ee Bwana. Kilindi kikipigia kelele Kilindi!"

214 Ni kiu cha namna gani tungalifikiria kilikuwa ndani yetu usiku wa leo? Sisi, kama watu Wapentekoste, tunaelekea wapi? Ni kiu cha aina gani kilicho ndani yetu? Ni kiu aina gani kilicho ndani yangu? Una kiu cha aina gani ndani yako? Usijaribu kutuliza hicho kiu kitakatifu cha Mungu.

215 Miaka mingi iliyopita, walipokuwa na dhahabu humu milimani. Nalisoma hadithi fulani, miaka mingi iliyopita, sijaisahau kamwe. Ilisema kulikuweko na m—mchunguza dhahabu aliyeondoka akaja humu mahali fulani ng'ambo ya pili ya milima humu, naye alikuwa akichunguza dhahabu, naye akaipata nyingi. Kisha akarudi, akiwazia; afikapo mjini, atakavyokuwa, shida zake zilikuwa zimekwisha kabisa. Na—naye—akajaribu ku—kusema, "Kesho nitaingia na nita . . ." Safari ya siku moja tu, naye angekuwa mjini, naye angekuwa na hiyo dhahabu. Naye alikuwa ameijaza magunia makubwa.

216 Basi alikuwa na mbwa. Silinganishi sasa huyo mbwa na Roho Mtakatifu, bali kwa maana natoa mfano. Lakini huyu mbwa . . .

217 Usiku kucha, huyo mchunguzi wa dhahabu alilala kitandani mwake, na—naye akaanza kuwazia, "Sasa, kesho nita—nitachukua dhahabu yangu yote, nami nitakuwa vile daima nilitaka kuwa. Da—da—daima nilitaka kuwa tajiri. Ni—nilitaka kuwa na vitu vizuri na kadhalika."

218 Ki—kisha huyu mbwa akaanza kuguruma, kwa sababu adui alikuwa akija. Naye—naye akatoka nje mle, akasema, "Nyamaza!" Basi mbwa akatulia. Mara tu alipoenda kitandani yule mbwa akaanza tena, akiruka tu nyororoni. Naye akaenda mlangoni tena, kasema "Nyamaza! Nakutaka ujue ya kwamba

kesho mimi ni tajiri, waona," na hizo zilikuwa doto zake kuu. Lakini mbwa akaanza kuguma tena.

219 Hatimaye akashushwa moyo, akaondoka akatwaa bunduki yake na kumpiga risasi yule mbwa, akamuua. Akasema, "Sikuhitaji tena, kwa vyo vyote. Kesho mimi ni tajiri. Nitakuwa tajiri kesho."

220 Naye akaweka bunduki yake pembeni, akaupa mlango kisogo, akalala. Kisha mtu aliyekuwa akimvizia, kwa siku nyingi, akapenya ndani na kumuua. Yeye hakutajirika, waona, alinyamazisha hiyo kengele ya maonyo iliyokuwa ikijaribu kumwambia ya kwamba maisha yake yalikuwa hatarini.

221 Basi, ndugu, dada, hautaweza kamwe ku...Usijaribu kamwe kunyamazisha huo wito mtakatifu moyoni mwako, unaona, kwa kujiunga na kanisa, kwa kukariri kanuni za imani, kwa kuwa mfuasi wa dhehebu fulani.

222 Kuna jambo moja tu linaloweza kuridhisha, huyo ni yule Mtu, Yesu Kristo. "Kama ayala aoneavyo shauku mto wa maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea kiu, Ee Mungu. Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu aliye hai!" Unaona, kuna kitu fulani ndani yako, kinachotaka kuona matendo ya Mungu. Nafsi yako inamwonea kiu. Usikome kabla hujapata hilo.

223 Usimwache mchungaji fulani akwambie, "Inakupasa tu kusalimiana naye kwa mkono, kujiunga na kanisa, ama kuwa mfuasi wa dhehebu *hili*." Usiangamize hiyo shauku takatifu. Ni onyo kwako. Siku yaja utakapofikia mwisho wa safari yako.

224 Kama maskini bibi fulani katika mji tunakotoka. Yeye alimwambia yule...Msichana mdogo alienda kanisani, msichana mzuri sana. Naye alikuwa anatembea barabarani. Alikuwa na nywele ndefu, mwajua, nazo nywele zake zilikuwa zimechanuliwa nyuma kama karibu kipande cha kitunguu kilichomenywa, na uso wake ulionekana kama...hamna rangi za kujirembesha. Na msichana huyu alizoea kumfanyia mzaha, kasema, "Kama hamngekuwa na huyo mhubiri baradhuli mliye naye kule," akinena habari zangu, kasema—kasema, "ungalionekana mtu mrembo. Bali unaonekana kama chombo kinachotoka kwenye duka la vitu vya kale." Na, lo, alimtia kwenye makaa ya moto, kila wakati alipomwona hivyo. Kasema, "Mchungaji wetu ni mtu mwenye maarifa mengi." Kasema, "A—a—anawajua. Hivyo, mbona unafanya hivyo? Hilo halimaanishi kitu, jinsi unavyovalia ama kuwazia." Inamaanisha! Biblia ya Mungu inasema inamaanisha. Tutaishi kwa kila Neno!

225 Kwa hivyo huyu msichana mdogo hakumjali huyo, akaendelea. Yeye ni mumishenari sasa.

226 Kwa hivyo huyu—maskini bibi huyu akapata ugonjwa wa zinaa, akafa. Rafiki yangu alimtia dawa ya kuhifadhi mwili alipokuwa mfu. Aliniambia, kasema...Baada ya kufa, yeye aliendelea kunuka hiyo dawa. Alikuwa na shimo upande mmoja,

ugonjwa wa zinaa. Hata wao hawaku-. . .Hata wazazi wake hawakujua shida yake. Naye akafa. Bali kabla hajafa . . .

227 Yeye alifundisha shule ya Jumapili. Na lile kundi lake dogo la shule ya Jumapili likaja, walitaka kumwona akienda Mbinguni, Malaika wakija kumchukua. Na mchungaji wake kule nje, akivuta sigara, akitembea huku na huko kwenye ukumbi wa hospitali. Nao wote walikuwa wataimba alipokuwa yuafa, mwajua. Walijua angekufa. Madaktari walisema yuafa, kwa hivyo wote walikuwa wakitarajia Malaika waje, wamchukue.

228 Mara tu alipokabiliana na hali halisi! Naam, alikuwa mfuasi mwaminifu wa kanisa, alikuwa mwalimu wa shule ya Jumapili, na mfuasi mwaminifu wa kanisa la dhehebu kubwa na nzuri. Bali alipoanza kung'angana, mauti yakamgusa; macho yake yakabenuka naye akasema, "Nimepotea!" Akasema, "Nimepotea! Nenda kamlete mchungaji!"

229 Akazima sigara yake, akaingia, akasema, "Basi, basi! Basi, basi! Tutamwita daktari akupe dawa ya usingizi."

230 Akasema, "Sitaki dawa yo yote." Kasema, "Wewe mlaghai! Nafa, nami naenda kuzimuni. Nimepotea kwa sababu ulishindwa kuniambia Ukweli. Nenda kamwite yule msichana wa Gooduse, kamlete hapa kwangu, upesi sana. Yeye ni wa kweli."

231 Ngoja mpaka utakapokabiliana na ukweli wa mambo wakati mmoja. Usithubutu. kunyamazisha hiyo shauku takatifu. Usiilipulie mbali kwa baadhi ya bunduki ya kisasa ya elimu yenye mitutu miwili. Sikiza hilo onyo la Roho Mtakatifu, usiku wa leo, akikuonya, "Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa Mimi." Naye ni Neno.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mdogo.

232 Nataka kunukuu Neno moja zaidi la Bwana Yesu, mnapowaza juu yake. Yesu alisema, katika Mathayo 5, "Heri wenye njaa na kiu ya haki." Hata ni heri kuwa na hicho kiu ndani yako. Je, umefikia mahali ambapo mipango yako yote imechafuliwa na udhehebu, na makundi madogo na ukabila, na kadhalika, kanuni dogo za imani, starehe, hupenda kujiunga na makanisa yaliyo vyumba vya kupanga, na kadhalika, kutoka kanisa moja hadi jingine? Je, Shetani amefaulu kukumwagilia hayo maji machafu, nawe unajiosha kwake, kama nguruwe katika hori lake? Huku hata hujui kituliza kiu halisi cha Mungu; kumwona Yeye, kitu halisi, kwa Roho Mtakatifu akiishi ndani yako, na akijidhihirisha. Ikiwa ndivyo—ikiwa ndivyo ulivyo usiku wa leo, iwapo ungali unamwonea kiu Mungu, hebu nikuambie:

> Damu imebubujika
> Ni ya Imanueli,
> Wakioga wenye taka
> Husafiwa kweli.

Ilimpa kushukuru
Mwivi mautini;,
Nami nisiye udhuru,
Yanisafi ndani.

Bwana, tangu damu yako
Kunisafi kale,
Nimeimba sifa Zake;
Taimba milele.

233 Kama una kiu hicho usiku wa leo, kumjua Mungu zaidi, na kumkaribia, je, waweza kuuinua mkono wako sasa huku kila kichwa kimeinamishwa, useme, "Niombee." Ee Mungu, tazama mikono hiyo!

234 Kote katika nchi ambazo zinafikiwa na matangazo haya sasa, kutoka Mashariki, Kaskazini, Magharibi, na Kusini, nyote katika vyumba hivyo, inueni mikono yenu kwa wachungaji na wo wote walioko huko, ya kwamba mnataka; ninyi, kitu fulani ndani yenu, kinamwonea kiu Mungu. Hicho kiu kitakatifu!

235 Usikiridhishe. Lo, unasema, "Ndugu Branham, ni—nilipaza sauti wakati mmoja. Nalicheza katika Roho." U—u—usichukue hilo. La.

236 Ngoja hata uradhi huo utakapokuja, ile Sehemu iridhishayo ya utimilifu wa Roho Mtakatifu itakapoingia, ndipo zile kengele za furaha za kupaza sauti, na kunena kwa lugha, na kucheza katika Roho, zitakuja. Haitakupasa kufanya hivyo kwa muziki. Utafanya hivyo utakapokuwa ukienda barabarani, kwa motokaa yako. Utafanya hivyo utakapokuwa ukifagia sakafuni. Utafanya hivyo utakapokuwa ukipigilia misumari ukutani, kwa kazi yako ya seremala. Po pote ulipo, hiyo Furaha isiyosemeka iliyojaa utukufu!

Sasa hebu na tuombe.

237 Baba mpendwa uliye Mbinguni! Ujumbe huu mdogo usiku wa leo, mrefu, wenye kuchosha, uliokokotwa, bali Mungu Mpendwa, na Roho Wako Mtakatifu aeleze ma—maana yake kwa kila moyo. Papa hapa kanisani humu, usiku wa leo, kulikuweko na ongezeko la hesabu ya mikono iliyoinuliwa juu, ukumbini mwote na kila mahali. Tu—tunaomba, Mungu mpendwa, kwa ajili yao. Lo, jamani, na Sehemu hiyo iridhishayo ya Mungu, ambayo ni Kristo, Tumaini la Utukufu, Tumaini la Uzima ndani yako, na imjie kila mmoja wao.

238 Toka upande hadi upande kote taifani, toka California, hata huko New York sasa, ambako ni asubuhi na mapema, wanasikiza kule; kule—kule New Hampshire, na huko chini Boston, na kule mbali Texas, kupitia Indiana, hata California, na kuzunguka. Ee Mungu, itazame mikono hiyo; tazama nini kilicho chini yao, Bwana, huyo moyo kule ambao unaona njaa na kiu.

239 Siku hii iliyopotoshwa, ambamo Shetani ameyapofusha macho ya watu, kujiunga tu na kanisa, na kusema, "Hilo tu ndilo unalohitaji." Nao wangali wanajiangalia wenyewe na kuona wanavyofanya, na shauku waliyo nayo kuwa kama ulimwengu.

240 Huku, Biblia inatuambia, "Tukiyapenda mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yetu."

241 Wazia tu Baba, jinsi yeye anavyoweza kupotosha hilo Neno halisi na la Kweli, jinsi wanavyoweza kusema, "Lo, tunaamini Biblia, bali si *Hili*. Hatuamini *Hili*. Tunaamini *Hii* ilikuwa kwa kizazi kingine. Tunamini *hili* ni *Lile,*" kwa sababu dhehebu fulani limegeuza bongo zao na kuziingiza kwenye shimo hilo la maji machafu.

242 Wakati, Yesu alisema, "Ye yote atakayeondoa Neno moja toka kwa *Hiki,* ama aongeze neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa katika kile Kitabu cha Uzima."

243 Mungu mpendwa! Waza kuhusu masikitiko kule Hukumuni, wakati ambapo watu ambao wameishi maisha mazuri, masafi, matakatifu, wakahudhuria kanisa kwa uaminifu iwezekanavyo, na wapotee.

244 Waza kuhusu hao Mafarisayo, jinsi, tangu utotoni, walifunzwa Neno, wakapitia shuleni na kila kitu, watakatifu (iliwapasa kuwa, ama wangalivawa kwa kupigwa mawe), na Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi."

245 Jinsi Israeli ilienda kule chini! Na hebu hili liwe onyo kwa Wapentekoste, Bwana, kote nchini. Jinsi ambavyo Musa, nabii, alivyoshuka kwenda Misri, kutimiza Neno la Mungu, kuwaletea nuru ya jioni! Jinsi walivyoona ile miujiza mikuu ya Mungu! Jinsi walivyomfuata, wakavuka Bahari ya Shamu, wakabatizwa katika yeye, wakaenda jangwani na kula chakula cha Malaika kilichoshuka kutoka Mbinguni. Kisha wakakataa kuchukua Neno lote, waliporudi kutoka Kadeshi-barnea, walipofika Kadeshi-barnea, kutoka ile—kutoka kwenye nchi ya ahadi, na kusema, "wao ni kama majitu; hatuwezi kufanya hivyo." Wakati, Mungu alisema, "Tayari nimewapa hiyo nchi"! Mpakani! Yesu alisema, "Hao, kila mmoja wao aliangamia. Wamekufa," wamepotea, bila Mungu, ingawa waliishafanya mambo haya yote. Walikwisha kuona miujiza hii; wakaifurahia, wakacheza huku na huko pwani, pamoja na Miriamu, walipopiga tari zao. Na ni watatu tu, kati ya milioni mbili, walioingia.

246 Tunatambua, Baba, kwamba wakati shahawa, zile chembechembe hai kutoka kwa kiume na kike, zinapokutana, kuna moja tu, toka kwa milioni moja, ambayo inakubalika. Mbegu moja kutoka kwa mwanamume hupata yai lililo tayari la mwanamke, mke, na milioni ya zingine huangamia.

247 Kuna milioni moja, milioni mbili, waliotoka Misri; wawili, Yoshua na Kalebu, waliingia katika nchi hiyo. Mmoja kutoka kwa milioni. Baba, na—natetemeka ninapowazia hilo. Waza,

kote ulimwenguni siku hizi, Wakristo milioni mia tano, hiyo ingekuwa watu mia tano ungalikuja usiku wa leo. Ee Mungu, hebu na tukumbuke ya kwamba kila Neno la Mungu hudumu, kama kumbukumbu. Hatuna budi kuliamini. Hatuna budi kulitii.

248 Nawe uliposema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwa katika Jina Lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Na, Mungu, Wewe ungali unaita, usiku wa leo, na ahadi ni mradi tu unaitana.

249 Na makasisi wamepotosha bongo za watu hao, na kuziongoza kwa Elimu ya shule ya theologia ya kidhehebu, kufikia mahali wanaposema, "Lo, amini tu." Shetani anaamini pia, bali hawezi kupokea Roho Mtakatifu. Yuda Iskariote alikuwa. . .alifanya yote hao we—wengine, hao wanafunzi waliyofanya, kuhubiri Injili; bali ilipofikia wakati wake wa kumpokea Roho Mtakatifu, akaonyesha alivyo hasa.

250 Mungu, na watu wa nchi hii usiku wa leo watambue ya kwamba, bila hilo tukio, wamepotea. Na iwe ni usiku wa leo ambapo mioyo yao itaridhishwa na Sehemu Yako, Bwana, tunapowakabidhi mkononi Mwako. Wao ni Wako, Bwana. Sisi tunahusika tu na Neno. Naomba ya kwamba wataamini kwa mioyo yao yote, na wajazwe na Roho Mtakatifu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

251 Lo, si Yeye ndiye Sehemu yenu inayotosheleza? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Lo, jamani! Mnampenda kwa mioyo yenu yote? ["Amina."—Mh.] Basi, Maneno haya wakati mwingine yanaumiza, bali hebu na tuimbeni katika Roho sasa, Mwaona, kila mmoja wetu sasa. Hebu tuamkuane kwa mikono na ndugu anayeketi karibu nawe, dada, na kusema, "Mungu akubariki, msafiri," tunapoimba tena. [Ndugu Branham asalimiana na watu.]

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

252 Sasa salimianeni kwa mikono ninyi kwa ninyi. Sasa hebuni tufunge macho yetu na tuimbe katika Roho, tumwinulie mikono yetu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Lo, si Yeye ni wa ajabu?

Wa ajabu, wajabu kwangu ni Yesu,
Mshauri, Mfalme, ni Mungu Mwenyezi;
Lo, huniokoa, hunilinda na haya na dhambi,
Wajabu ni Mkombozi msifuni!
Wajabu wajabu, kwangu ni Yesu,
Mshauri, Mfalme, ni Mungu Mwenyezi;
Huniokoa, hunilinda na haya na dhambi,
Wajabu ni Mkombozi msifuni!

253 Lo, je, mmefurahia ujuzi wenu na Kristo? [Kusanyiko linafurahi, "Amina."—Mh.] Si yeye ni wa ajabu? Si Yeye anaridhisha?

Kapotea, kanipata, huru na hukumu,
Yesu hutoa uhuru, wokovu tele,
Huniokoa, hunalinda na haya na dhambi,
Wajabu ni Mkombozi msifuni!

Lo, wajabu, kwangu ni Yesu,
Mshauri, Mfalme ni Mungu Mwenyezi;
Lo, huniokoa, hunilinda na haya na dhambi,
Wajabu ni Mkombozi msifuni!

254 Je, unaamini hiyo ni kulingana na Maandiko? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Biblia ilisema, "Pigeni makofi. Mpigieni Bwana kelele za shangwe." Mwajua, daima nilitaka kucheza muziki. Binti yangu, Rebeka, anajifunza piano. Mvulana wangu mdogo anajifunza tarumbeta. Bali ni—nilijifunza kinanda cha nyuzi kumi. [Ndugu Branham anaanza kupiga makofi.]

Wa ajabu, wa ajabu, kwangu ni Yesu,
Mshauri, Mfalme ni Mungu Mwenyezi;
Huniokoa, hunilinda na haya na dhambi,
Wa ajabu ni Mkombozi msifuni!

Je, mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri sana,
Njooni ambapo matone ya umande wa neema
  yanang'ara;
Tuangazie kote usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri sana,
Njoo ambapo matone ya umande wa neema
  yanang'ara.
Tuangazie kote usiku na mchana;
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

255 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, "Yesu, Nuru ya ulimwengu," na makutano pia wanavumisha pamoja naye.—Mh.] Mwabudu Mungu kwa kila kitu ulicho nacho.

Watakatifu watakapoingia mle,
Watakatifu watakapingia mle,
Bwana, nataka kuwa katika hesabu hiyo
Watakatifu watakapoingia mle.

Lo, watakapomvika taji kuwa Bwana wa mabwana,
Watakapomvika taji kama Bwana wa mabwana,
Bwana, nataka kuwa katika hesabu hiyo
Watakapomvika taji kama Bwana wa mabwana.

Lo, wakati jua litakapokataa kuwaka,
Wakati jua litakapokataa kuwaka,
Bwana, nataka kuwa katika hesabu hiyo
Jua litakapokataa kuwaka.

256 Je, mnampenda? [Makutano wanasema, "Amina."—Mh.] Sasa nashangaa kama miguu yenu iliongoka, hamchezi tena, kule nje ulimwenguni? Mwaona? Hebu tupige chini kwa miguu yetu, kwa Bwana, kwa Bwana. Je, mikono yako imeongoka, hauibi tena? Midomo yako imiongolewa, hausemi uongo tena? Usiingize dini kichwani mwako tu, ijaze mwili mzima. Hivyo tu. Inachukua mtu mzima. Hiyo ni kweli. Hebu tupige chini kwa miguu yetu.

Wakati watakatifu watakapoingia mle,
Wakati watakatifu watakapoingia mle,
Bwana, nataka niwe katika hesabu hiyo
Watakatifu watakapoingia mle.

Lo, wakati watakatifu watakapoingia mle,
Wakati watakatifu watakapoingia mle,
Bwana, nataka niwe katika hesabu hiyo
Watakatifu watakapoingia mle.

Basi natuinueni mikono yetu.

Wakati watakatifu watakapoingia mle,
Wakati watakatifu watakapoingia mle,
Bwana, nataka niwe katika hesabu hiyo
Watakatifu watakapoingia mle.

Watakapomvika taji kuwa Bwana wa mabwana,
Watakapomvika taji kuwa Bwana wa Mabwana,
Bwana, nataka kuwa katika hesabu hiyo
Watakapomvika taji kuwa Bwana wa vyote.

257 Je, hamumpendi? [Kusanyiko linafurahia, "Amina! Utukufu! Haleluiya"—Mh.]

Basi tutatembe Nuruni (Yeye ni Nuru, mwajua), Ni Nuru nzuri,
Huja ambapo matone ya umande wa neema yanangara;
Vema, tuangazie kote usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

258 Je, mnaamini Yeye ni Nuru ya ulimwengu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini? Paulo alisema, "Nikiimba, nitaimba katika Roho. Nikiabudu, nitaabudu katika Roho." Waona, cho chote ufanyacho, fanya katika Roho. Hiyo ni kweli. Naye Roho hulihuisha Neno. Sivyo? Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

Enyi watakatifu wa Nuru tangazeni,
Yesu, Nuru ya ulimwengu;
Neema na rehema katika Jina Lake,
Yesu, Nuru ya . . .

Basi tufanye nini?

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
Huja ambapo matone ya umande wa neema yanang'ra;
Tuangazie kote usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

259 Nasikitika kwa kuwachanganyisha enyi wachezaji, hivyo, bali mimi huchukuliwa upesi. Sijui vingine ila kuabudu. Hivyo ndivyo ufanyavyo. Naam, bwana. Ninafurahia nafasi hii, Ndugu Mack, kuja kushirikiana nanyi na kanisa lenu hapa usiku wa leo, watu hawa wote wema.

260 Nanyi mlioinua mikono yenu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, natumaini ya kwamba mtamwona Mchungaji Mack hapa, ama baadhi yao, na muingie katika chumba kimoja hapa. Na hebu kumbukeni tu, Mungu aliponena Neno hapo mwanzo, akasema, "iwe," ilipaswa kuwa! Naye akasema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa." Unaona, haina budi kutendeka. Njooni mkamtembelee mchungaji wenu hapa, na mkae pamoja naye anapohubiri Injili.

261 Basi hebu tuuimbe tena huo wimbo mzuri wa kale, naupenda huo, "Tutatembea Nuruni."

262 Yesu alisema, "Mimi ni Nuru," nanyi mko ndani Yake. Mnaona? Je, mnaingiaje ndani Yake? Kunjiunga Naye? La. Kusalimiana? La. Ubatizo wa maji? La. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, ambao ni Mwili wa Kristo." Na katika Mwili huo mna karama tisa zinazotenda kazi kwa Mwili wa mahali hapo, kanisa la mahali hapo. Hiyo ni kimitume, kama nilipata kujua habari zake. Hiyo ni kweli.

Kwa hivyo tutadumu Nuruni, katika Nuru nzuri,
Huja ambapo matone ya umande wa neema yanaangaza,
Tuangazie kote usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

*Kiu* SWA65-0919
(Thirst)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Septemba 19, 1965, katika Grantway Assembly of God kule Tucson, Arizona, Merekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org